BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,018,116,895/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



UKURASA 3

**Daktari** matatani madai ya kunajisi mtoto wa miaka 8


# Nipashe

Alhamisi Julai 28, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581020

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




MASTRAIKA WAMVURUGA ZORAN

UKURASA 24

# TUCTA yawasilisha hoja mpya serikalini



Ni kuhusu nyongeza mishahara, yataka asilimia 15 kima cha juu... Uk. 2

UKURASA WA 2

### MAELEKEZO MAALUMU KESI KINA MDEE KESHO

MAHAKAMA Kuu, Masjala Kuu, Dar es Salaam inatarajia kutoa maelekezo maalum kesho katika shauri lililofunguliwa na Mbunge wa Viti Maalumu, Halima Mdee na...

UKURASA WA 4

### HAKIMU AGOMA KUJITOA KESI YA ZUMARIDI

HAKIMU Mkazi, Monica Ndyekobora wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza, amekataa kujitoa katika kesi ya Mchungaji Diana Bundala, maarufu Mfalme Zumaridi...

UKURASA WA 4

### KINANA ATOA NENO KODI WAFANYABIASHARA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Abdulrahman Kinana, ameagiza wafanyabiashara wadogo na wa kati wasitozwe kodi nyingi kabla ya kuanza biashara...

## Onyo ulaji wa vibudu, nyama mbichi kuepuka homa ya mgunda

UKURASA 3

# Ajali iliyoua, kujeruhi yaibua mambo mapya

UKURASA 2

MICHEZO SPORTPESA YAMWAGA MABILIONI YANGA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# TUCTA yawasilisha hoja mpya serikalini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SHIRIKISHO la Vyama vya wafanyakazi nchini (TUCTA), limewasilisha serikalini hoja zake kuhusu nyongeza za mshahara huku likipendekeza kiwango cha kima cha juu cha mshahara kisipungue asilimia 15.

Pamoja na kuwasilisha hoja hizo, shirikisho hilo pia limesema limebaini baadhi ya kada na taasisi za umma hazijaguswa na nyongeza hizo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Rais wa TUCTA, Tumaini Nyamhokya, alisema wamewasilisha hoja zao kwa maandishi kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala bora.

Alitaja mambo ya msingi yaliyozingatiwa katika hoja zao kuwa ni namna nyongeza ya mshahara ilivyofanyika na umekuwa utaratibu ambao haukumridhisha mtumishi yeyote wa umma.

"Kwa sababu tumeona kiwango cha chini ni asilimia 23.3 lakini akitafutwa wa kima cha juu ana asilimia 0.6. Hii ni tofauti kubwa ambayo haijawahi kutokea na utaratibu wa namna hii haufanyiki.

"Tukumbuke Mheshimiwa Rais (Samia Suluhu Hassan) alilenga kuongeza mishahara na hakuwa amelenga kuwatoa watu wa daraja fulani kuwapeleka mahali pengine lakini kama ni nyongeza ya mshahara inagusa kila ngazi ya mshahara kwa mtumishi wa umma. Suala hili tumeliwasilisha," alisema. Pia alisema kuna kada za utumishi na taasisi za umma ambazo watumishi wake hawajaguswa na nyongeza ya mshahara.

"Kwa mfano tunaona watumishi wengi wenye mishahara binafsi. Hii pia imegawanyika, kuna wale ambao wana elimu ya darasa ya saba ukiuliza wanasema ni watu ambao kwenye mfumo wa serikali hawasomeki. Hakuna mpangilio wa kiwango chao cha mshahara kwa hiyo hawakuguswa kabisa.

"Ukiwatazama kwenye idara za afya, watendaji wa kata na mitaa, nyongeza ya mshahara haikuwagusa kabisa. Pia kuna wale wenye mishahara binafsi walihama taasisi moja na kwenda nyingine akakuta kule cheo chake kinachosomeka kimuundo hakipo kwa hiyo akahamishwa kwa mshahara binafsi na wao pia hawakuguswa kabisa na nyongeza ya mshahara.

"Kwa hiyo tunaona kumekuwa na ubaguzi mkubwa na sababu hatuioni ni nini iliyofanya ngazi zingine za mshahara kukosa nyongeza," alisema.

Nyamhokya aliongeza kuwa kuna baadhi ya taasisi wamejaribu kufuatilia kama Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) hawana nyongeza kabisa ya mshahara.

"Watu wa TRC hawajaguswa pia na wenyewe ni sekta ya umma. Tunaona jambo hili halijakaa vizuri ndiyo maana tumewapa wenzetu warudi wakalifanyie kazi," alibainisha. Rais huyo alisema hata kiwango cha mishahara cha Sh. 70,000 bado kikitazamwa si kiwango halisia kinachomtoa mtumishi kwenye adha za maisha kulinganisha hali halisi ya sasa.

Alisema pendekezo lao ni jinsi walivyokuwa wakiongezwa mishahara miaka ya nyuma, hivyo itazamwe zaidi asilimia badala ya kutazama kiwango cha fedha.

"Na hiyo tofauti ya asilimia 23.3 kwa kiwango cha chini cha mshahara na asilimia 0.6 kwa kiwango cha juu cha mshahara tumeona imepungua mno. Imekwenda kwenye mtu mwenye 'almost' kwenye sifuri. Tumependekeza angalau mwenye kima cha juu asipungukiwe nyongeza ya asilimia 15 wakati huyo mwenye kima cha chini akiwa ameongezewa asilimia 23.3," alisema.

Nyamhokya alisema wanasubiri majibu ya serikali kuhusu hoja hizo. Alipotafutwa na Nipashe ili kujua kauli ya serikali baada ya kupokea hoja hizo, Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema: "Tutawajulisha."

Juzi, Msigwa alisema serikali imeanza majadiliano ya awali na TUCTA katika kikao ambacho kilihudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwamo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama.

Julai 22, mwaka huu, serikali iliahidi kutoa ufafanuzi juu ya hoja iliyozungumzwa na wafanyakazi kuhusu nyongeza ya mshahara ya kima cha chini iliyotokea kwenye mishahara ya mwezi huu.

Mei, mwaka huu, Rais Samia aliahidi kuongeza mshahara kwa watumishi wa umma na baadaye aliridhia mapendekezo ya nyongeza ya mshahara ya kima cha chini kuwa asilimia 23.3 na kwamba Sh. trilioni 1.59 zitatumika kwa ongezeko hilo.

Katika sherehe za Mei Mosi, mwaka huu, TUCTA iliomba kima cha chini cha mshahara kiongezwe hadi Sh.1, 100,000 kwa mwezi kwa mfanyakazi kutokana na kupanda kwa gharama za maisha.



Halima Mdee na wenzake wakitoka mahakamani. **PICHA: MAKTABA**

# Ajali iliyoua, kujeruhi yaibua mapya

**Na Abdallah Bakari na Baraka Jamali,** MTWARA

GARI lililopata ajali juzi eneo la Mjimwema, Manispaa ya Mtwara Mikindani na kusababisha vifo vya watu 13 lilibeba wanafunzi wa shule tatu tofauti, imebainika.

Wanafunzi hao ni kutoka shule ya King David ambao ndio wamiliki wa gari lenye namba za usajili T 207 CTS, Shule ya Msingi Singino na Shule ya Sekondari Mikindani.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Tarafa ya Mikindani, Octavian Lyapembile, aliwataja wanafunzi hao kuwa ni pamoja na mwanafunzi wa Shule ya Msingi Singino, William Mrope wa darasa la nne, ambaye alifariki dunia.

"Ni kweli kwenye lile gari kulikuwa na wanafunzi wa shule zingine. Wa sekondari ambao wamejeruhiwa ni Walda Rashidi (12) , Waseme Omari (16), Latifa Abasi (14) wa kidato cha tatu, Address Emanuel (15) wa kidato cha pili na Veronica Christopher (15) wa kidato cha kwanza" alisema Lyapembile.

**SABA WAPEWA RUFANI**

Majeruhi 16 wa ajali hiyo wanaendelea vizuri huku saba wakihamishiwa Hospitali ya Rufani ya Ndanda na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Jana, Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Ligula, Dk. Clemence Haule, alisema majeruhi wanaendelea vizuri na wengine wamepewa rufani kutokana na hali zao kuwa mbaya na kuhitaji utaalam zaidi.

Aliwataja majeruhi waliopewa rufani kwenda Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kuwa ni Waseme Omari (25) aliyevunjika mguu, Mary Tarimo (6) mwenye maumivu kwenye uti wa mgongo, Nairat Juma (12) aliyepata majeraha mkononi, Lorreta Ruzangi (12) na Hanifa Ramadhani (6) waliojeruhiwa mikono.

Waliohamishiwa Ndanda ni Address Emanuel (15) na Ratifa Abasi (14) wote wamevunjika miguu.

Pia aliwataja majeruhi wanaoendelea na matibabu Ligula kuwa ni Mairini Msigwa, Batham Robert, Bianka Abdallah, Josephine Thomas, Megani Msigwa, Saidi Ramadhani, Akson, Veronica Rashidi na Chrispine Jackison.

Wakati huo huo, miili ya wanafunzi wawili wa familia moja waliofariki dunia katika ajali hiyo, Johari na Emanuel Simon, iliagwa jana katika Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Newala na itasafirishwa kwenda mkoani Dodoma kwa mazishi.

# Maelekezo maalumu kesi kina Mdee kesho

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu, Masjala Kuu, Dar es Salaam inatarajia kutoa maelekezo maalum kesho katika shauri lililofunguliwa na Mbunge wa Viti Maalumu, Halima Mdee na wenzake 18 la kupinga kuvuliwa uanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Mahakama hiyo, ilifikia hatua ya kupanga siku hiyo, Julai 29, 2022 kwa kuwa imeshapanga jaji wa kusikiliza shauri hilo, Cyprian Mkeha.

Kutokana na hatua hiyo shauri litatajwa mbele ya Jaji Mkeha na pia anatarajiwa kutoa maelezo hayo muhimu katika shauri hilo.

Mdee na wenzake walifungua shauri hilo namba 36/2022 Julai 22, 2022 wakiomba mahakama hiyo ipitie mchakato na uamuzi wa kuwafukuza uanachama na kisha itoe amri tatu.

Katika shauri hilo, wabunge hao wanaiomba mahakama itengue mchakato na uamuzi wa kuwavua uanachama na pia iwalazimishe CHADEMA kuwapa haki ya kuwasikiliza.

Pia wanaomba amri ya zuio dhidi ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kutokuchukua hatua yoyote hadi malalamiko yao yatakapotolewa uamuzi.

Pamoja na mambo mengine, wabunge hao wanadai kuwa mchakato na uamuzi wa kuwafukuza uanachama haukuzingatia matakwa ya kisheria na misingi ya haki, wakidai kuwa hawakupewa haki ya kusikilizwa.

Katika kiapo cha Mdee, anadai kuwa Novemba 25, 2020 CHADEMA walimtumia barua ya maelezo ya makosa yake kupitia mtandao wa WhatsApp na kumtaka ahudhurie kikao cha Kamati Kuu kilichopangwa kufanyika Novemba 27, 2020, ikiwa ni taarifa ya siku mbili pekee.

"Kutokana na hasira na vitisho vya usalama wake na kauli za Katibu Mkuu wa CHADEMA kwa umma kuwa ni wasaliti matokeo yake wanachama walianza kutoa vitisho kwa kiwango cha kushutumiwa na hata kuitwa Covid- 19," kilieleza kiapo cha Mdee.

Mdee anadai kuwa kutokana na hayo aliingiwa na hofu ya kushambuliwa na wanachama wa chama hicho waliochochewa na kauli za viongozi wao akiwamo Katibu Mkuu, John Mnyika.

Pia Mdee anadai kwamba baada ya kula kiapo, Novemba 24, 2020, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika alimtaja yeye na wenzake 18 kama wasaliti.

## HABARI KITAIFA

# Daktari matatani kwa madai ya kunajisi mtoto wa miaka minane

**Na Jenifer Gilla**

MTU mmoja anayedhaniwa kuwa daktari, anashikiliwa na polisi katika kituo cha Gogoni Luguruni, Kibamba mkoani Dar es Salaam kwa tuhuma za kumnajisi mtoto wa kike wa miaka minane (jina linahifadhiwa).

Akizungumza jana na Nipashe, baba wa mtoto aliyefanyiwa kitendo hicho, (jina linahifadhiwa), alisema walifungua kesi na kupewa namba KIM/RB/2875/2022, iliyoandikwa kosa la kujaribu kubaka.

Baba mzazi huyo, akisimulia jambo hilo kama alivyoelezwa na mwanawe, alisema siku ya tukio mtoto wake akiwa anacheza nje ya nyumba ya mtuhumiwa, alimwita na kumwingiza ndani kisha akamvua nguo na kumfanyia ukatili huo.

Alisema licha ya mtoto huyo kupiga kelele kuwa anaumia, daktari huyo hakujali akaendelea na ukatili huo kisha akamwambia asimwambie mtu yeyote.

Kwa mujibu wa baba huyo, baada ya kupewa onyo hilo, mtoto aliogopa kutoa taarifa nyumbani badala yake alimwambia mtoto mwenziwe aliyekuwa anacheza naye ambaye naye alikwenda kumsimulia mama yake mkasa huo.

"Mtoto wangu alimwambia mtoto wa jirani kwamba daktari kambaka. Sasa yule mtoto hakuvumilia akaenda kumwambia mama yake na kwa kushirikiana na majirani wengine, walimwita mtoto wangu wakamhoji akasema yote ndipo wakamwita mke wangu na kumwambia," alibainisha.

Baada ya mke wake kupata taarifa hiyo na kumweleza, alisema walikwenda kituo cha Polisi Gogoni na kufungua kesi, kisha wakatakiwa kumpeleka hospitalini kupimwa tena.

Baba huyo alisema walimpeleka mtoto huyo Hospitali ya Kimara kwa ajili ya vipimo na baada ya majibu kutoka, daktari aliyewahudumia akawaambia kuwa hawezi kuwapa majibu kwa siku hiyo kwa kuwa ana wagonjwa wengi anawaowahudumia na kuwataka warudi baada ya siku saba.

Alisema mkuu wa kituo cha polisi alimwambia arudi tena hospitalini ndipo daktari huyo akamwambia kuwa arudi kesho yake.

"Wakati anajaza, hakujaza kile ambacho kiliandikwa kwenye karatasi ya majibu. Kuna daktari mwenzie akawa anamwambia wewe ukijaza hivyo unaweza ukamfunga mtu. Sasa nikawa najiuliza kama majibu yanaonyesha mtoto kachezewa kwa nini yasiandikwe. Mimi nikapiga picha yale majibu sahihi," anasimulia.

Pia alisema baada ya daktari kuandika alipiga picha taarifa ambayo iliandikwa matokeo ya maabara 'being raped which/ as the father reports quoting' (amebakwa kama baba alivyomsikia mtoto wake akisema).

Alisema kilichomshangaza ni kilichoandikwa kwenye fomu ya polisi kuwa "being molested by a known adult person to them" (amedhalilishwa na mtu mzima anayejulikana).

# Onyo ulaji wa vibudu, nyama mbichi kuepuka homa ya mgunda

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KUTOKANA na kuibuka kwa ugonjwa wa homa ya mgunda mkoani Lindi, serikali imewataka Watanzania kula nyama iliyopikwa vizuri kwa nyuzi joto 70 huku ikionya ulaji wa wanyama wasioliwa ikiwamo panya.

Aidha, wamesisitizwa kununua nyama iliyochinjwa kwenye machinjio na kuuzwa kwenye mabucha yaliyosajiliwa na Bodi ya Nyama nchini.

Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Hezron Nonga, akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapo, alisema panya sio mnyama anayetakiwa kuliwa na binadamu kwa kuwa ni benki ya vimelea vya ugonjwa huo.

"Mimi kama daktari wa masuala ya wanyama, hivyo naelekeza jamii ya Watanzania tuepuke kula panya sababu ni chanzo cha maradhi mengi, huyu panya ni benki ya vimelea vya ugonjwa huu wa mgunda, pia wachukue tahadhari ya popo wanaoingia kwenye nyumba ni hatari wana magonjwa mengi," alisema.

Alisema, kuna uvumi unaowatia hofu Watanzania kwamba wasile nyama kutokana na kuibuka kwa ugonjwa huo jambo ambalo sio kweli, kinachotakiwa ni kupikwa na kuchomwa vizuri.

Prof. Nonga alisema pia maziwa, mayai na maji ya kuchemshwa yanapaswa kupikwa vyema.

"Njia pekee ya maambukizi ya mgunda ni kula nyama ambayo haijaiva vizuri, nitoe rai kwa wananchi kutokutaharuki na kuacha kula nyama na badala yake wahakikishe nyama wanayokula imeiva vizuri," alisisitiza. Alisema ulaji wa nyama ndiyo njia rahisi ya kukabiliana na utapiamlo kutokana na takwimu kuonyesha kuwa nchini Tanzania mtu mmoja anakula kilo 15 kwa mwaka huku mapendekezo ya kimataifa ni kilo 50 kwa mwaka. "Ulaji wa nyama bado tupo chini hivyo ni muhimu kula nyama, lakini ni nyama ipi ni ile ambayo kwanza imechinjwa kwenye machinjio ya serikali, kwa kuwa imepimwa na wataalamu na imepigwa muhuri kuuzwa kwenye maduka ambayo yamezingatia vigezo vya Bodi ya Nyama, lakini hiyo nyama ipikwe na kuiva vizuri," alisema.

Alisema utafiti uliofanyika nchini unaonyesha kuwa maambukizi ya ugonjwa huo yalishawahi kutokea kwa binadamu na wanyama.

"Inaonyesha kwa wanyama wa kufugwa ni ng'ombe, mbuzi, nguruwe, mbwa na paka katika mikoa ya Morogoro, Kilimanjaro, Tanga, Dar es Salaam, Katavi, Mwanza, Singida, Kagera na Mbeya waligundulika kuwa na maambukizi," alisema.

"Matibabu ya ugonjwa huu kwa wanyama ni dawa ya antibiotic aina ya doxycline au penicillin, tunasisitiza mnyama wako apate chanjo, kutochunga maeneo ya maambukizi kama vile kwenye hifadhi za wanyamapori, kudhibiti panya kwenye mazingira ya mifugo."

Kwa upande wake, Msajili wa Bodi ya Nyama nchini, Dk. Daniel Mushi, alisema bodi hiyo inaendelea kufanya ukaguzi kwenye mabucha mbalimbali nchini na kuyafunga yasiyokidhi vigezo na yatakayobainika kuuza nyama isiyothibitishwa na wataalamu.

"Nawasihi Watanzania wasile nyama za vibudu kwa kuwa ni hatari mnaweza kupata maambukizi ya ugonjwa huu," alisema.

Bank of India (Tanzania) Ltd.

Relationships beyond banking

Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2022

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

**WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2022**
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Jun-22 | Robo Mwaka iliyopita 31-Mar-22 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 1,963 | 1,983 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 13,693 | 10,994 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 49,219 | 53,283 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 1,849 | 1,675 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 10,669 | 27,890 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 84,392 | 74,812 |
| 12 | Mali Nyingine | 2,665 | 3,246 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,916 | 1,460 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **167,366** | **175,343** |
| B. | B. DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 55,567 | 66,682 |
| 18 | Amana za Wateja | 69,331 | 68,101 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 80 | 110 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 25 | 25 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 2,260 | 2,246 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 1,990 | 371 |
| 28 | Madeni | - | - |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **129,253** | **137,536** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **38,113** | **37,807** |
| C. | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,500 | 21,500 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 2,130 | 1,631 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 13,739 | 14,470 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 744 | 206 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **38,113** | **37,807** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 6,708 | 6,987 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 6,449 | 6,438 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 1,219 | 875 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 22.77% | 21.56% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 7.53% | 8.51% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 68.54% | 56.15% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali | 50.42% | 42.67% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 86.93% | 89.46% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -7.33% | 4.85% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -4.55% | 2.46% |

**TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2022**
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka wa sasa 30-Jun-22 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Jun-21 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Jun-21 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 3,431 | 2,528 | 6,467 | 5,602 |
| 2 Gharama za Riba | 1,240 | 1,149 | 2,432 | 2,380 |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **2,191** | **1,379** | **4,035** | **3,222** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | (5) | - | (5) | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 344 | 367 | 581 | 391 |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **236** | **143** | **372** | **260** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za | 62 | 45 | 89 | 85 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 174 | 98 | 283 | 175 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **1,364** | **1,322** | **2,715** | **2,498** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 567 | 504 | 1,234 | 991 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | 797 | 818 | 1,481 | 1,507 |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **724** | **(167)** | **1,116** | **593** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 187 | 219 | 373 | 438 |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **537** | **(386)** | **743** | **155** |
| **11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| **12 Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa robo ya** | **537** | **(386)** | **743** | **155** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 34 | 30 | 34 | 30 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 100 | (72) | 69 | 14 |
| 15 Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.72% | -0.41% | 1.31% | 0.73% |
| (ii) Wanahisa | 5.66% | -4.25% | 3.93% | 0.84% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 37.20% | 49.49% | 39.70% | 42.61% |
| (iv) Zinazozalisha | 6.02% | 4.04% | 5.45% | 4.70% |

**TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2022**
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo Juu ya bei ya Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo mwaka ya sasa 2022** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka 01.04.2022** | **21,500** | - | **14,675** | **1,631** | - | - | **37,806** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 537 | - | - | - | 537 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (499) | 499 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mikopo iliyofutwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | | | (230) | | | | (230) |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka 30.06.2022** | **21,500** | - | **14,483** | **2,130** | - | - | **38,113** |
| **Robo Mwaka iliyopita 2022** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka 01.01.2022** | **21,500** | - | **14,377** | **1,631** | - | - | **37,508** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 206 | - | - | - | 206 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mikopo iliyofutwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | 93 | - | - | - | 93 |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka 31.03.2022** | **21,500** | - | **14,676** | **1,631** | - | - | **37,807** |

**TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2022**
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Jun-22 | Robo Mwaka iliyopita 31-Mar-22 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Jun-21 |
|---|---|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 724 | 393 | 1,116 | 593 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 394 | 448 | 966 | 740 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (9,925) | (3,851) | (13,776) | 2,903 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (9,885) | 6,232 | (3,653) | 1,206 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 8,517 | (4,751) | 3,766 | (534) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 1,028 | (1,401) | 625 | (205) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 2,713 | (968) | 630 | 3,960 |
| | - Kodi Iliyolipwa | (187) | (187) | (373) | (438) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za*** | ***(6,621)*** | ***(4,085)*** | ***(10,699)*** | ***8,225*** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (0) | (282) | (289) | (170) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | ***(0)*** | ***(282)*** | ***(289)*** | ***(170)*** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | - | - | - | - |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | **(6,621)** | **(4,367)** | **(10,988)** | **8,055** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 40,727 | 45,094 | 45,094 | 32,540 |
| | **Robo Mwaka** | **34,106** | **40,727** | **34,106** | **40,595** |

**BANK OF INDIA (TANZANIA) LTD**
**DAR ES SALAAM**

**BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2022**

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| **Mr. Antaryami Sarangi** Mkurugenzi Mtendaji | Imesainiwa | 22.07.2022 |
| **Mr. Mahadhil M.Karwani** Mkuregenzi wa Fedha | Imesainiwa | 22.07.2022 |
| **Mr. Allen Richard** Mkaguzi Mkuu wa Ndani | Imesainiwa | 22.07.2022 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| **1. Mr. Suitbert Kageuka - Mkurugenzi** | **Imesainiwa** | **22.07.2022** |
| **2. Dr. Paul Kato - Mkurugenzi** | **Imesainiwa** | **22.07.2022** |

216963601

# Hakimu agoma kujitoa kesi ya Zumaridi

**Na Richard Makore,** MWANZA

HAKIMU Mkazi, Monica Ndyekobora wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza, amekataa kujitoa katika kesi ya Mchungaji Diana Bundala, maarufu kama Mfalme Zumaridi kama walivyooomba mawakili wake.

Mapema mwezi huu, jopo la mawakili wa utetezi, likiongozwa na Steven Kitare, liliwasilisha kusudio lao la kumkataa hakimu huyo ingawa hawakutaja sababu za msingi kutaka kufanya hivyo.

Kesi hiyo namba 10 ambayo imeendelea kuzua mjadala katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, jana iliendelea katika mahakama hiyo na kuvuta umati wa watu.

Jana, kesi hiyo ilifanyika ili kutolewa uamuzi mdogo wa ombi la mawakili wa utetezi la kumtaka hakimu ajitoe kutokana na kutokuwa na imani naye.

Katika uamuzi huo mdogo, Hakimu Ndyekobora aliwaambia mawakili hao kwamba hawezi kujitoa katika kesi hiyo kwa sababu hakuna sababu za msingi za kisheria.

Baada ya uamuzi huo, Wakili Kitare alisimama na kuomba kesi hiyo isiendelee kwa shahidi kuendelea kutoa ushahidi kutokana na kasoro za matakwa ya kisheria.

Kesi hiyo iliahirishwa jana huku upande wa utetezi ukipanga kuwasilisha mahakamani hoja zao kwa kuwa awali waliziwasilisha ofisini kwa hakimu.

Katika kesi hiyo, Zumaridi na wenzake wanane wanakabiliwa na shtaka la kufamya fujo na kuzuia askari polisi pamoja ofisa ustawi wa jamii kufanya kazi yao.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Agosti 10, mwaka huu, itakapoendelea kwa wakili wa utetezi kuwasilisha hoja zao za kumkataa hakimu huyo mbele ya mahakama.



Mmoja wa kinamama wanaojishughulisha na kazi ya kukaanga dagaa na samaki katika Kisiwa cha Mandakelenge wilayani Nkasi akipokea mtungi wa gesi kutoka kwa Waziri wa Nishati, January Makamba (kushoto), alipofika kisiwani hapo kusikiliza kero za wananchi, kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia na kukagua usambazaji umeme katika Kisiwa cha Mandakelenge ambacho kinapata umeme baada ya serikali kupitisha nyaya za umeme chini ya maji katika Ziwa Tanganyika. Kulia ni Mbunge wa Nkasi Kaskazini, Aida Khenan. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kinana atoa neno kodi wafanyabiashara jela

**Beatrice Shayo na Maulid Mmbaga,** SUMBAWANGA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Bara, Abdulrahman Kinana, ameagiza wafanyabiashara wadogo na wa kati wasitozwe kodi nyingi kabla ya kuanza biashara.

Kinana aliyasema hayo jana wakati akihutubia wananchi mjini hapa akiwa kwenye ziara ya kikazi inayolenga kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo na utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya chama.

Alisema kumekuwa na tabia kwa baadhi ya taasisi kutoza utitiri wa kodi wafanyabiashara wadogo wanaoanza biashara jambo linalodidimiza badala ya kuwaendeleza.

Kinana aliagiza wafanyabiashara wadogo na wa kati wasitozwe kodi nyingi kabla ya kuanza biashara ili wamudu uendeshaji wa biashara.

"Serikali, watumishi wa serikali na viongozi, sekta ya binafsi inaanza na wafanyabiashara wadogo, hivyo lazima tuwasaidie wafanyabiashara, tuwapunguzie kero za kufanya biashara, sijui mmenielewa hapa? Wako wakurugenzi, madiwani na wenyeviti wa halmashauri mhakikishe hili linazingatiwa," alisema.

Kinana alisema sekta binafsi haipo kwa ajili ya kumkomoa mwananchi bali kumsaidia ndiyo maana Rais Samia Suluhu Hassan amedhamiria kupunguza kero hizo ili kuwainua wafanyabiashara.

"Wenye kuuza mitumba, chakula, wenye kuuza karanga tuwapunguzie kero. Mtu anataka kufungua biashara ana fedha kidogo Sh. 500,000 au Sh 50,000 kabla ya kufungua biashara anaambiwa alete karatasi ya usafi, karatasi ya osha, karatasi ya kumkagua, karatasi ya makisio ya kodi, mazingira nao. Sasa huo mtaji utakuwa umebaki tena? Si utakuwa umekwisha?" alihoji.

Kinana alisema wasubiri kwanza mtu afanye biashara na akishapata fedha ndipo atatakiwa kulipa hizo kodi na si kulipa kabla ya biashara kuanza.

"Mfanyabiashara anataka kufungua biashara, taasisi nyingi zinamtoza kodi. Hii nchi ina mamlaka nyingi za kutoza kodi na si kuendeleza watu maskini,"alisema.

Kinana alisema kila anayekuja dukani kwako anakudai hakuna anayekuja kuuliza una shida gani ili usaidiwe biashara ikue badala yake wanaulizia kodi tu.

"Tulipe kodi sawa lakini wasianze na kodi kabla ya biashara. Mama lishe anataka kuuza chakula chake kidogo, anaambiwa alipe kodi mtaji wenyewe ni Sh. 50,000. Analipa kodi gani badala ya kukopeshwa yeye ndiyo anailipa serikali,"alisema Kinana.

Aidha Kinana alisema sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inaeleza kama biashara haijafika milioni tano haupaswi kulipa kodi.

Awali, akizungumza akiwa kata ya Paramawe Wilaya ya Nkasi, Kinana aliwauliza kinamama kama wamejitokeza kwa wingi kugombea nafasi mbalimbali na kusisitiza kuwa wanawake wanapewa kipaumbele kwa sababu ni zaidi ya nusu ya Watanzania na wamekuwa waaminifu.

"Wakigombea nafasi ni lazima muwape kipaumbele kwa sababu kinamama ni waaminifu. Kinababa pamoja na mimi tuna kautapeli tapeli kidogo kweli. Kinamama ni watenda haki na kinababa wanapenda dhuluma dhuluma," alisema Kinana.

# Waajiri wabanwa sheria za kazi

**Na Frank Monyo**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako, amewataka waajiri kutekeleza sheria za kazi, ikiwamo Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi, ili kuzalisha kwa tija na kuepuka migogoro.

Alitoa agizo hilo jana alipofanya ziara katika maeneo ya kazi Dar es Salaam akiwa ameambatana na viongozi na maofisa wa taasisi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu zinazosimamia sheria mbalimbali za kazi.

Baada ya kufanya ziara katika viwanda vitatu vinavyojishuhulisha na utengenezaji wa rangi na mabomba, Prof. Ndalichako alibainisha kuwa wamiliki hao wanajitahidi kutekeleza matakwa ya sheria na maelekezo ya serikali, lakini kuna upungufu ambao unapaswa kurekebishwa.

"Kuna baadhi ya wafanyakazi hawana vifaa kinga na wengine wanapewa lakini hawavitumii. Inabidi wasimamiwe na kuna baadhi ya viwanda tulivyotembelea tumebaini uwapo wa kiwango cha juu cha kelele ambazo zinaweza kuathiri wafanyakazi endapo hatua madhubuti za kuwakinga hazitachukuliwa," alisema Prof. Ndalichako.

"Kwa hiyo nawaagiza OSHA (Mamlaka ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi) kuja katika viwanda hivi kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa kina na kushauri jinsi ya kuboresha mifumo ya kuwalinda wafanyakazi dhidi ya vihatarishi mbalimbali vya usalama na afya," alisisitiza.

Kuhusu mifuko ya hifadhi ya jamii, Prof. Ndalichako alifafanua kuwa ofisi yake inapata malalamiko ya wastaafu na kwamba changamoto zao zinatokana na waajiri wao wa zamani kutotimiza wajibu wao wa kuwasilisha michango kwenye mifuko husika.

"Serikali tumeamua kufuatilia kwa karibu juu ya michango ya wafanyakazi tunahitaji wazee wapate mafao yao bila usumbufu. Tayari kwenye baadhi ya viwanda nimegundua hakuna uwiano kati ya idadi halisi ya wafanyakazi na kiwango cha michango kinacholipwa," alisema Prof. Ndalichako.

# TANGAZO

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

**AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**
*benki kwa maendeleo yako*

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30.06.2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka Mwaka wa sasa 30-Jun-22 | Robo Mwaka Mwaka iliyopita 31-Mar-22 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 15,985 | 13,458 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 11,727 | 8,567 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 44,496 | 46,850 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 405 | 446 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 41 | 88 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 35 | 23 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 0 | 0 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 80,187 | 78,982 |
| 12 | Mali Nyingine | 14,255 | 13,208 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 39 | 39 |
| 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 14,301 | 14,828 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **181,469** | **176,490** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 1,134 | 1,285 |
| 18 | Amana za Wateja | 123,718 | 118,813 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana Maalumu | 61 | 130 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 6 | 5 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 4,728 | 3,297 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 958 | 916 |
| 27 | Dhima Nyingine | 16,484 | 17,129 |
| 28 | Madeni | 6,823 | 5,630 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **153,912** | **147,206** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **27,557** | **29,284** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 27,797 | 27,797 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (10,819) | (12,432) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (1,317) | 411 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 11,896 | 13,508 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **27,557** | **29,284** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 765 | 616 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 13,303 | 11,993 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 6,591 | 5,618 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 73 | 73 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 15.2% | 16.6% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 15.4% | 14.2% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 67.9% | 69.1% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 47.6% | 47.8% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 68.9% | 71.6% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 3.9% | -2.0% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 2.8% | -1.4% |

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI
## KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.06.2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka sasa 30-Jun-22 | Robo ya mwaka Linganishi 30-Jun-21 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30-Jun-21 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 6,470 | 5,796 | 13,402 | 11,815 |
| 2 Gharama za Riba | (1,655) | (2,177) | (3,392) | (4,349) |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **4,815** | **3,619** | **10,010** | **7,467** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (1,826) | (552) | (1,856) | (1,989) |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,711** | **1,401** | **3,321** | **2,553** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 106 | 89 | 185 | 153 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 1,320 | 924 | 2,436 | 1,693 |
| 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | !"#$%& 0 |
| 6.4 Mapato Mengine | 286 | 388 | 701 | 708 |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **(6,603)** | **(6,163)** | **(12,791)** | **(12,329)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (3,649) | (3,052) | (7,122) | (6,155) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 7.3 Gharama Nyingine | (2,954) | (3,111) | (5,668) | (6,174) |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(1,903)** | **(1,694)** | **(1,317)** | **(4,298)** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 176 | 0 | (0) | 0 |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(1,727)** | **(1,694)** | **(1,317)** | **(4,298)** |
| **11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **12 Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(1,727)** | **(1,694)** | **(1,317)** | **(4,298)** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 392 | 413 | 392 | 413 |
| 14 Mapato kwa Hisa | (62) | (76) | (47) | (192) |
| **15 Idadi ya Matawi** | **18** | **18** | **18** | **18** |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -3.9% | -4% | -1.5% | -5% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -24.3% | -27% | -9.3% | -34% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 101.2% | 123% | 96.0% | 123% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 15.3% | 14% | 15.9% | 15% |

## BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.06.2022

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Mr. Silvest Arumasi *(Mkurugenzi Mtendaji)* | | |
| Mr. Arnold Makanda *(Afisa Mkuu wa Fedha)* | | |
| Mr. Chemo Mutani *(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)* | | |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| 1. Mr. Ernest Massawe | | |
| 2. Prof. Josephat Daniel Lotto | | |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA
## KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30.06.2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Jun-22 | Robo Mwaka iliyopita 31-Mar-22 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30-Jun-21 |
|---|---|---|---|---|---|
| **I:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (1,903) | 586 | (1,317) | (4,298) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | - Hasara Katika Mali | 487 | 484 | 971 | 1,226 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (1,205) | (1,274) | (2,478) | 4,597 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | 0 | (0) | 0 | 0 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 4,685 | (2,460) | 2,225 | 2,763 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 2,355 | (5,763) | (3,408) | (6,230) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 2,447 | (400) | 2,047 | 3,967 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 1,285 | 2,787 | 4,072 | (1,595) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (127) | 0 | (127) | (124) |
| | - Mengineyo (bainisha) | (411) | (436) | (848) | (349) |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | **7,613** | **(6,476)** | **1,137** | !"#$%& **(43)** |
| **II:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (168) | (140) | (307) | (198) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mengineyo (bainisha) | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | **(168)** | **(140)** | **(307)** | **(198)** |
| **III:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 0 | 5,960 | 5,960 | 0 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 | 0 | (0) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mengineyo (bainisha) | (556) | (544) | (1,101) | (455) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **(556)** | **5,415** | **4,859** | **(455)** |
| **IV:** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 6,890 | (1,201) | 5,689 | (696) |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 19,195 | 20,395 | 20,395 | 32,668 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **26,084** | **19,195** | **26,084** | **31,972** |

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30.06.2022

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2022** | **27,797** | **2,432** | **(12,101)** | **4,857** | **5,888** | **28,874** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | (1,317) | 0 | 0 | **(1,317)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | -72 | 0 | 72 | **-** |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | 1353 | -1353 | 0 | **0** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| **Salio la mwisho wa mwaka 30.06.2022** | **27,797** | **2,432** | **(12,136)** | **3,504** | **5,960** | **27,557** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2021** | **10,984** | **2,432** | **(5,627)** | **3,684** | **16,992** | **28,465** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | (4,298) | 0 | 0 | **(4,298)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Miamala na wanahisa | 11,427 | 5,565 | 0 | 0 | (16,992) | **(0)** |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | (1,225) | 1,225 | 0 | **(0)** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| **Salio la mwisho wa mwaka 30.06.2021** | **22,411** | **7,997** | **(11,151)** | **4,909** | **(0)** | **24,167** |




216962901

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ajali hizi zitaondoa maisha ya watu mpaka lini?

**WIMBI** la ajali limeendelea kuikumba nchi na kupoteza maisha ya Watanzania wengi wakiwamo watoto ambao ni tegemeo la taifa la kesho.

Ajali hizo zimekuwa zikitokea mfululizo wakati machungu ya ajali zingine yakiwa hayajaisha kwenye mioyo ya watu.

Ajali nyingi zinazotokea uchunguzi wa awali unaonyesha chanzo ni mwendo kasi na ubovu wa magari.

Mwendo kasi wa madereva umekuwa ukisababisha ajali nyingi kwa sababu linapotokea jambo lolote kwa dharura barabarani, dereva anashindwa kuhimili gari na matokeo yake ajali kutokea na kusababisha vifo.

Ajali iliyotokea juzi na kuondoa maisha ya watoto wetu, wakiwamo wa familia moja, imegusa mioyo ya watu wengi. Mzazi kupoteza watoto wake wote kwa wakati mmoja ni jambo la kuhuzunisha sana.

Watoto wasiokuwa na hatia wanaaga wazazi wao asubuhi kwenda shule, baada ya muda taarifa zinakuja hawapo tena duniani.

Ajali hii inakumbusha iliyowahi kutokea miaka ya nyuma ambayo iliondoa uhai wa wanafunzi wengi na wengine kupata ulemavu.

Serikali pamoja na kuchukua hatua mbalimbali za kudhibiti ajali zisiendelee kutokea, kwa kuwataka wamiliki kuweka vidhibiti mwendo na kufanyia magari yao ukaguzi wa mara kwa mara, lakini hilo pia halija saidia.

Pamoja na Kikosi cha Polisi Usalama Barabarani kufanya operesheni kadhaa za kudhibiti ajali hiyo, lakini hali hiyo inaendelea kujitokea mara kwa mara, sio kwa mabasi ya abiria, binafsi, ya serikali na mabasi ya shule, ajali nyingi zinaendelea kushuhudiwa nchini.

Hivi juzi juzi tu, kulitolewa agizo la kufanyika ukaguzi wa magari yote ya shule yanayobeba wanafunzi na ukaguzi huo ulibaini kuwa mengi yalikuwa mabovu yanayotakiwa kufanyiwa marekebisho na matengenezo.

Hatufahamu kama ukaguzi mwingine ulifanyika kubaini kama agizo la kuyatengeneza lilitekelezwa ili kuepusha ajali kwa watoto wetu.

Taarifa za polisi kuhusu ajali iliyotokea juzi na kupoteza maisha ya wanafunzi, zinaeleza kuwa gari walilokuwa wakisafirishiwa watoto hao lilifeli breki na kuishia kutumbukia kwenye korongo.

Kufeli kwa breki kunamaanisha kuwa gari hilo halikufanyiwa ukaguzi, au kama lilifanyiwa kulikuwa na uzembe wa kuliacha litembee barabarani na kuhatarisha maisha ya watu.

Wakati ajali kama hizi ziliposhamiri miaka ya nyuma kwa mabasi ya abiria, serikali ilibadili utaratibu wa ratiba kwa yaliyokuwa yakisafiri usiku na yote kutakiwa kuanza safari asubuhi. Hii ilitokana na kubainika kuwa baadhi ya madereva waliokuwa wakisinzia na matokeo yake kusababisha ajali.

Tatizo lingine ni madereva kujaza abiria kuliko uwezo wa magari yao, hata inapotokea ajali husababisha wengi kupoteza maisha.


Kuna umuhimu mkubwa wa kufanya ukaguzi kila siku kabla dereva hajaingia barabarani kuhakikisha usalama wa gari lake.

Madereva pia kuwa makini wawapo barabarani kwa sababu wanabeba roho za watu wengine. Wahenga wanasema haraka haraka, haina baraka. Na mwendo kasi hata siku moja haujawahi kumuacha dereva salama.

Tuchukue hatua kudhibiti ajali hizi, tusiendelee kushuhudia vifo vya watu wasiokuwa na hatia kwa sababu ya ajali.

Mungu ibariki Tanzania na atuepushe na janga hili la ajali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tutambue hizo dalili nane za mgunda na kuchukua hatua

Na Sabato Kasika

**MLIPUKO** wa ugonjwa wa mgunda ambao sasa umekuwa ni mjadala miongoni mwa Watanzania baada ya kuibuka wilayani Ruangwa mkoa wa Lindi na kudaiwa kusababisha vifo vya wale waliokumbwa nao.

Ugonjwa huo pia unajadiliwa kwenye vyombo vya habari, ikiwamo mitandao, kutokana na kwamba unaonekana kuwa mpya, ingawa serikali imeweka wazi kuwa si mpya kwa vile umewahi kutoka mkoani Kigoma.

Tayari serikali imeshasema kuwa homa ya Mgunda au Leptospirosis ni ugonjwa unaosababishwa na bakteria ambapo kwa mujibu wa Waziri wa Afya Ummy Mwalimu, umekuwa ukiathiri wanadamu na wanyama.

Lakini, pamoja na kuwapo kwa mjadala kuhusu ugonjwa huo, ninadhani ni vyema sasa Watanzania wakaelekeza nguvu katika kutambua dalili za ugonjwa huo, ili wachukue tahadhari pale wanapoubaini.

Wizara ya Afya imeshaweka wazi kuwa, ugonjwa huo una dalili nane ambazo ni homa kali, kuumwa kichwa, maumivu makali, uchovu wa misuli, kupata homa ya manjano hasa kwenye macho na macho kuvilia damu.

Dalili nyingine za ugonjwa huo ambazo Watanzania wanatakiwa kuzijua, zinatajwa na Wizara ya Afya kuwa ni kukohoa na kutokwa damu puani na kichefuchefu kinachoambatana na kutapika, kuharisha na tumbo kuuma.

Hivyo, badala ya kuendelea kujadili ugonjwa huo, ninadhani ingekuwa ni vyema jamii ingejikita, pia kufahamu dalili hizo ili pale unapojitokeza, iwe rahisi kuchukua hatua sahihi za kuhakikisha hauleti maafa.

Kwa kuwa bakteria wanaosababisha ugonjwa huo huenezwa kupitia mkojo wa wanyama walioambukizwa, na kwamba wanaweza kuingia ndani ya maji au udongo na kuishi huko kwa wiki hadi miezi, suala la tahadhari ni la muhimu.

Watanzania ni wakulima na wafugaji na inaelezwa kuwa aina nyingi tofauti za wanyama wa porini na wa nyumbani wakiwamo ng'ombe, nguruwe, farasi, mbwa, jamii ya panya na wanyama wa porini, hubeba bakteria.

Lakini, kwa kuwa inaelezwa kuwa wanyama hao wanapopata maambukizi, wanaweza kuwa hawana dalili za ugonjwa huo na kuendelea kutoa bakteria kwa kuendelea au kila baada ya muda kwa miezi michache hadi miaka kadhaa.

Jambo la muhimu ni kila mmoja, mtu mzima kutambua dalili za ugonjwa huo zilizotolewa na wizara, lakini kuwa makini, kwa kuwa bakteria wanaweza kuingia mwilini kupitia ngozi au utando wa macho, pua au mdomo.

Inaelezwa kuwa hayo yanaweza kutokea ikiwa ngozi ina mikwaruzo, hivyo suala la kuwa makini ni la muhimu kuanzia kuchukua kila aina ya tahadhari na pia kutambua dalili za ugonjwa huo.

Jamii isichukulie kuwa ugonjwa huo ni wa eneo hilo, kwani Waziri wa Afya anasema ulishawahi kuibuka mkoani Kigoma na sasa umetua mkoani Lindi, ambako ni mbali zaidi ya kilomita 1,000 kutoka Kigoma.

Kwa ugonjwa huo, ni vyema kutumia msemo wa Kiswahili kuwa; 'ukiona mwenzio ananyolewa na wewe tia maji', hivyo wakati upo mkoani Lindi, ni vyema wananchi wa maeneo mengine kuchukua tahadhari.

Ikumbukwe kuwa watu wanasafiri kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine, hivyo ni rahisi aliye na ugonjwa huo kupelekea kwingine kirahisi. Njia nzuri ni kujua dalili zake na kuchukua tahadhari.

Ninaamini kwamba, kujua dalili za ugonjwa huo ni hatua muhimu ambayo itamfanya mtu kwenda hospitali au kituo cha kufanyiwa vipimo unapoona mwili wake hakuna usawa, kabla hali haijawa mbaya.

Tunaambiwa na Wizara ya Afya kuwa, awamu ya kwanza ya ugonjwa ambayo ni homa, baridi, maumivu ya kichwa, maumivu ya misuli, kutapika, na kuhara, mgonjwa anaweza kupona kwa muda lakini akaugua tena. Kwa mujibu wa wizara hyo, homa ya Mgunda inatibiwa na dawa aina ya antibiotics, kama vile doxycycline au penicillin, ambayo inapaswa kutolewa mapema katika kipindi cha ugonjwa huo.

Hivyo, kwa maelezo hayo, ni wazi kwamba, suala la kujua dalili za ugonjwa huo lina uzito wake, ambapo bila kuzijua, mtu anaweza kuugua na kudhani mwingine na kumbe ndio wenyewe, kwa hiyo ni vyema kuwa makini.

# Mgogoro Anglikana watinga vyombo vya kisheria

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MGOGORO wa Kanisa la Aglikana Tanzania umechukua sura mpya baada ya aliyekuwa Katibu Mkuu wake, Dk. Mecka Ogunde, kufungua shauri kulishtaki Baraza la Wadhamini katika Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA).

Hali hiyo inatokana na Baraza la Wadhamini wa kanisa hilo kumwondoa madarakani Dk. Ogunde kwa madai ya kuwa nje ya ofisi kwa muda mrefu mapema mwezi Juni mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kusikilizwa kwa shauri hilo, wakili wa mlalamikaji Willson Ogunde, alisema wamefikia maamuzi hayo baada ya Baraza la Wadhamini wa Kanisa la Anglikana Tanzania, kushindwa kufikia makubaliano na mteja wake.

"Shauri tulilofungua ni CMA/DOM/84/2022 na mteja wangu ambaye alikuwa Katibu Mkuu wa Kanisa la Aglikana Tanzania analalamikia ajira yake kusitishwa bila kufuatwa sheria na bila sababu ya msingi, hivyo kukosa haki zake za msingi hadi sasa.

"Leo (jana) ilikuwa mara ya kwanza kusikilizwa lakini wenzetu wa upande wa pili wameleta hati kinzani, mapingamizi ambayo tumeomba muda kwenda kuyapitia ili kuja kutolea majibu kabla ya Agosti 10, mwaka huu, ambapo shauri hili litasikilizwa tena," alisema.

Pia alisema mteja wake ameamua kufungua shauri hilo baada ya vikao vya ndani ya kanisa kushindwa kumpatia haki anayostahili.

"Kanisa wamefanya mazungumzo na mteja wangu lakini hatujapata mwafaka. Kila mara wamekuwa wakipanga vikao ambavyo hawaji na kila mara wanatupiga chenga na kutukwepa. Tumeamua kufungua shauri hili katika chombo hiki cha kisheria ili kupata haki ya mteja wangu kwani tayari alishatumikia nafasi yake kwa muda wa miaka minne na miezi miwili na mkataba wake ulikuwa wa miaka mitano," alisema.

Juni, mwaka huu, wakati sakata hilo limeibuka, Askofu Mkuu wa Kanisa hilo, Dk. Maimbo Mndolwa, aliongoza ibada ya kumsimika Canon Bethuel Mlula kuwa Katibu Mkuu katika ibada iliyofanyika kwenye Kanisa la Mtakatifu Paulo Mtume kwa Mataifa wilayani Kondoa.

Akizungumza katika ibada hiyo, Dk. Mndolwa alisema hakukuwa na mgogoro isipokuwa uamuzi ulifanyika kupitia kikao cha Nyumba ya Maaskofu ambacho kiliazimia kumwondoa na kumpata katibu mkuu mpya ili kazi ya Mungu isonge mbele. Askofu mkuu pia alikanusha taarifa zilizosambaa kuwa kanisa hilo limeingia kwenye mgogoro kati yake na katibu mkuu kutokana na maandalizi ya kuelekea uchaguzi wa Askofu Mkuu.

"Kanisa la Anglikana Tanzania liliamua kupitia taratibu zake zote kwamba nafasi ya katibu mkuu ni nafasi ya mtu aliyeamriwa wa daraja takatifu na si 'mlei' kwa sababu hiyo kinachotangulia kwanza ni vile viapo vya huduma takatifu. Maaskofu walitazama hayo na kuamua kuwa tunahitaji mabadiliko," alisema Askofu Dk. Mndolwa.

Alitaja sababu ya kufikia uamuzi huo kuwa ni katibu mkuu huyo kutoonekana mara nyingi ofisini kwa sababu familia yake iko Australia, hivyo muda mwingi amekuwa akiutumia kusafiri na kusababisha mambo mengi ya kanisa kukwama.

Kuhusu katibu mkuu huyo kutolipwa na kusitishiwa mkataba kabla ya muda, Dk. Mndolwa alisema kanisa haliangalii mikataba ya kawaida bali mikataba ya kiroho kwa kuwa mhusika anawaangalia wananchi.

"Mkataba wa ajira sisi makasisi na maaskofu hatuingii kwa ajira yoyote ila tunaingia kama watumishi. Hatulipwi mishahara ila tunalipwa posho, kwa hiyo kwa yeyote anayesimama akiwa na kola akadai kwamba ana ajira huyo kwa kweli hayupo katika 'order' ya Kianglikana," alisema.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Imperial Marketing and Communications (IMC), Murtaza Ebrahim (katikati aliyeshika tuzo), akiwa na wafanyakazi wa kampuni hiyo wakionyesho tuzo waliyoshinda kwenye kipengele cha kampuni bora kwa ubunifu wa masoko wakati wa Tuzo za Tanzania Marketers Awards zilizofanyika mwishoni mwa wiki na kuandaliwa na Chama cha Sayansi na Masoko Tanzania (Tanzania Marketing Science Association – TMSA) jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake watakiwa kuuepuka utegemezi

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

WANAWAKE nchini wametakiwa kujihusisha na ujasiriamali utakaowaingizia kipato cha kujikimu kiuchumi na familia zao ili kuondoa utegemezi na kunyanyasika.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Dawati la jinsia mkoa wa Morogoro, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Mwanaidi Lwena, wakati wa warsha ya wanawake na maendeleo yenye lengo la kuhimiza wanawake kujitambua na kujitathmini.

Alisema familia zimeingia kwenye migogoro kwa sababu wanawake wengi wamebaki kuwa tegemezi kwa wanaume zao, badala ya kutafuta fursa za kufanya shughuli za ujasiriamali na kujikuta wakiendelea kunyanyasika.

"Tumewekeana mikakati na wanawake hawa tuliokutana nao kwamba sasa ni lazima kutoa taarifa katika dawati letu wanapoona wanafanyiwa ukatili," alisema.

Mariam Mattao ni mshauri wa wanawake masuala ya saikolojia, alisema vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia vimesababisha baadhi ya wanawake kuathirika kisaikolojia kwa kukosa utulivu wa nafsi katika familia zao

Alisema muda mwingi wanajikuta wakiishi kwa hofu ya waume zao na kusababisha kushindwa kufanya shughuli zao za kiuchumi na kuwataka kusimama imara katika kutafuta haki zao bila uwoga na kutafuta msaada wa kisheria inapohitajika

Baadhi ya washiriki akiwamo, Consolata Chuwa, aliiomba serikali kupitia wizara ya maendeleo ya jamii kuendelea kuwawezesha wanawake kiuchumi ili kufikia malengo ya usawa wa kijinsia na kutokomeza kabisa vitendo vya ukatili.

Naye, Ofisa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Morogoro, Kutaiwa John, alisema taratibu na sheria za serikali katika kumuwezesha mwanamke kiuchumi zipo wazi na kuwataka wanaweke hao kujitokeza na kujiunga katika vikundi, ili kupatiwa mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na serikali.

# Watanzania washauriwa kupima afya ya kinywa, meno kila wakati

**Na Gwamaka Alipipi**

WATANZANIA wametakiwa kuwa na utaratibu wa kupima afya ya meno na kinywa kila wakati badala ya kusubiri wanapoumwa au kupata maumivu.

Rai hiyo ilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Daktari Bingwa wa magonjwa ya kinywa na meno, Gilbert Tarimo, wakati wa uzinduzi wa kliniki ya kwanza ya kisasa ya meno na kinywa iitwayo Afya Bora Complete Dentistry Ltd, ambayo itakuwa mahususi katika kutoa suluhisho la kudumu la matatizo ya meno nchini.

Dk. Tarimo alisema Watanzania wengi wamekuwa na tabia ya kwenda hospitali kutibu meno pindi wanaposumbuliwa na maumivu ya meno na kwamba wengi huhitaji kung'oa jino linalosumbua hali ambayo inaweza kusababisha matatizo mengine katika mwili.

Dk. Tarimo alisema utafiti unaonyesha kuwa magonjwa mengi yakiwamo shambulio la moyo, kisukari, kiharusi, maambukizi katika mapafu yana uhusiano wa karibu na maambukizi yaliyopo katika kinywa. Alisema katika kliniki hiyo wanafanya uchunguzi wa afya ya kinywa na mgonjwa anapewa ripoti ya kila kitu kuhusu kinywa chake na hatua anazopaswa kuchukua ili kuboresha afya yake zaidi.

Dk. Tarimo alisema: "Tunataka kuimarisha afya ya kinywa, kuimarisha afya yote ya mwili wa mgonjwa, hapa tumejikita zaidi katika kukinga, kudhibiti magonjwa ya kinywa, pia tunatibu afya ya binadamu kupitia kinywa chake."

Mtendaji Mkuu wa kiliniki hiyo, Dk. Donna Ngirwa, alisema kituo hicho kitajikita zaidi kueneza elimu kuhusu uhusiano uliopo kati ya afya ya kinywa na afya ya binadamu kwa ujumla.

Alisema watu wengi wanaishi vizuri kwa kula chakula kizuri na kufanya mazoezi, lakini wanakosa afya ya kinywa.

"Kwa kuwa watu wengi hawana bima ya meno, mpango wa afya bora ya meno utatoa huduma bure za uchunguzi wa meno, usafishaji wa meno, vipimo vya X-ray na punguzo la asilimia 20 kwa tiba kamili ya meno."

Dk. Ngirwa alisema kliniki hiyo inatoa huduma zote za meno ikiwamo usafishaji, kuweka meno bandia, mpangilio wa meno na huduma nyinginezo za tiba ya meno.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI

216965001

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
Tarehe 27/07/2022

## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Alhamisi tarehe **28-07-2022** kampuni ya **HAINAN INTERNATIONAL LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **DODOMA**, gari hilo lenye namba za usajili:

**T 175 DFN**
**T 168 DFN.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 18.00, Urefu - mita 2.80, Urefu - mita 5.00**

3. Njia itakayotumika: **DAR ES SALAAM** hadi **DODOMA** kupitia **MOROGORO**. Gari itasafiri muda wa mchana tu (**kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni**)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

# TANGAZO

International Commercial Bank (Tanzania) Limited.

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30.06.2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | ROBO MWAKA YA SASA | ROBO MWAKA ILIYOPITA |
|---|---|---|---|
| | | 30.06.2022 | 31.03.2022 |
| A. | ***MALI*** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 1,679 | 1,624 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 7,621 | 7,083 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 18,071 | 18,674 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 1,118 | 4,945 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 2 | 59 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 19,852 | 21,501 |
| 12 | Mali Nyingine | 15,785 | 15,833 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,046 | 1,062 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **65,173** | **70,781** |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 0 | 1,160 |
| 18 | Amana za Wateja | 34,115 | 38,931 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 162 | 162 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | 0 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,470 | 1,292 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 61 | 61 |
| 27 | Dhima Nyingine | 3,010 | 2,855 |
| 28 | Madeni | - | - |
| 29 | ***JUMLA YA DHIMA*** | **38,819** | **44,461** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **26,354** | **26,319** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 28,937 | 28,937 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 3,036 | 3,283 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (18,249) | (18,525) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 778 | 773 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 11,851 | 11,851 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | ***JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA*** | **26,354** | **26,319** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 443 | 389 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 8,402 | 7,051 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 1,774 | 1,396 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 40.44% | 37.18% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 36.43% | 29.58% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 67.28% | 60.62% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 30.46% | 30.38% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 59.90% | 63.75% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -23.04% | -9.63% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -12.02% | -4.45% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30.06.2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | ROBO MWAKA YA SASA | ROBO MWAKA LINGANISHI LA MWAKA ULIOPITA | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA | LIMBIKIZO LINGANISHI LA MWAKA ULIOPITA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 30.06.2022 | 30.06.2021 | 30.06.2022 | 30.06.2021 |
| 1 | Mapato ya Riba | 1,032 | 1,019 | 2,625 | 2,093 |
| 2 | Gharama za Riba | 420 | 428 | 878 | 851 |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | ***612*** | ***592*** | ***1,747*** | ***1,242*** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | 0 | - | 2 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 273 | 338 | 202 | 338 |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **1,230** | **105** | **2,167** | **266** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 31 | 12 | 46 | 20 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 27 | 24 | 27 | 58 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 1,172 | 69 | 2,095 | 188 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **1,556** | **1,385** | **2,922** | **2,684** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 591 | 565 | 1,152 | 1,170 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 122 | 113 | 175 | 126 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 843 | 707 | 1,594 | 1,388 |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **12** | **(1,026)** | **791** | **(1,516)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 6 | - | 12 | - |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **6** | **(1,026)** | **778** | **(1,516)** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **6** | **(1,026)** | **778** | **(1,516)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 53 | 58 | 53 | 58 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 0 | (51) | 39 | (76) |
| 15 | Mapato kwa Hisa zilizochujwa | 0 | (51) | 39 | (76) |
| 16 | **Idadi ya Matawi** | 4 | 4 | 4 | 4 |
| | ***BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI*** | | | | |
| 1 | Uwiano wa Faida kabla ya kodi na Wastani wa mali | 0.03% | -6.04% | 2.24% | -4.32% |
| 2 | Uwiano wa Faida baada ya kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 0.09% | -16.75% | 6.02% | -12.25% |
| 3 | Uwiano wa matumizi yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 68.82% | 123.13% | 60.97% | 113.79% |
| 4 | Uwiano wa mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali zinazozalisha | 5.83% | 5.08% | 8.44% | 5.12% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30.06.2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | ROBO MWAKA YA SASA | ROBO MWAKA ILIYOPITA | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA | LIMBIKIZO LINGANISHI LA MWAKA ULIOPITA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 30.06.2022 | 31.03.2022 | 30.06.2022 | 30.06.2021 |
| | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 12 | 779 | 791 | (1,516) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| | - Hasara Katika Mali | 363 | (41) | 322 | 468 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 1,377 | 668 | 2,045 | 513 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (5,976) | (4,289) | (10,264) | 7,272 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 333 | 231 | 564 | (63) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 48 | 478 | 526 | (98) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (6) | (6) | (12) | - |
| | -SMR | 296 | 150 | 446 | 323 |
| | - Mengineyo | 31 | - | 31 | (36) |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | ***(3,522)*** | ***(2,030)*** | ***(5,551)*** | ***6,864*** |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (74) | (675) | (750) | (844) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | | | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | 603 | (203) | 400 | 2,738 |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **529** | **(878)** | **(349)** | **1,894** |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | 1,035 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | **-** | **-** | **-** | **1,035** |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **(2,993)** | **(2,908)** | **(5,901)** | **9,793** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Mwaka/Mwaka | 11,448 | 14,356 | 14,356 | 8,753 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Mwaka/Mwaka | **8,455** | **11,448** | **8,455** | **18,546** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30.06.2022

| **Mwaka wa sasa** | **Mtaji wa Hisa** | **Tengo la Ziada ya Jumla** | **Mapato Yaliyobakizwa** | **Ziada ya Kisheria** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2022** | **28,937** | **11,851** | **(17,489)** | **2,255** | **25,554** |
| Marekebisho ya mwaka uliopita | | | 22 | - | **22** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | | | 778 | | **778** |
| | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | |
| Miamala na wanahisa | | | | | |
| Gawio lililolipwa | | | | | |
| Ziada ya Kisheria | | | (782) | 782 | |
| Tengo la Ziada ya Jumla | | | | | |
| Mengineyo | | | | | |
| | | | | | |
| Nyongeza ya Mtaji | - | | | | |
| **Salio la mwisho wa kipindi 30.06.2022** | **28,937** | **11,851** | **(17,470)** | **3,036** | **26,354** |
| | | | | | |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2021** | **28,937** | **-** | **(11,316)** | **7,455** | **25,076** |
| Marekebisho ya mwaka uliopita | | | (338) | - | (338) |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | | | (11,035) | | (11,035) |
| | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | |
| Miamala na wanahisa | | | | | |
| Gawio lililolipwa | | | | | |
| Ziada ya Kisheria | | | 5,201 | (5,201) | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | | | | | |
| Mengineyo | | | | | |
| | | | | | |
| Nyongeza ya Mtaji | | 11,851 | | | 11,851 |
| **Salio la mwisho wa kipindi 31.12.2021** | **28,937** | **11,851** | **(17,489)** | **2,254** | **25,554** |

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zile zile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

**Saini:**

**SANJEEV ANAND**
Ofisa Mtendaji Mkuu
Tarehe: 26 Julai 2022

**GEORGE MSAMBAZI**
Mkuu wa Fedha
Tarehe: 26 Julai 2022

**JOHN MWAKASONDA**
Mkaguzi Mkuu wa Ndani
Tarehe: 26 Julai 2022

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006,na zinaonesha hali halisi.

**Saini:**

**ALFRED MKOMBO**
Mjumbe wa Bodi
Tarehe: 26 Julai 2022

**HASHIMAH BINTI ISMAIL**
Mjumbe wa Bodi
Tarehe: 26 Julai 2022

# Utafiti athari COVID-19 kutoa matokeo Septemba

**Na Romana Mallya**

DAKTARI wa Magonjwa ya Ndani ikiwamo Moyo na Mapafu katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MMH), Elisha Osati, amesema utafiti kuhusu madhara ya muda mrefu yatokanayo ya ugonjwa wa UVIKO-19, umefikia hatua ya kati.

Akizungumza na Nipashe jana, Dk. Osati alisema mwishoni mwa mwezi Septemba, mwaka huu, watakuwa na cha kusema kuhusu utafiti huo unaoendelea.

Katika ripoti maalum iliyofanywa na gazeti hili mwezi Oktoba, mwaka 2021 ikiangalia namna ugonjwa huo ulivyogharimu maisha ya madaktari, Dk. Osati alifunguka na kusema kuwa kwa wakati huo alikuwa kwenye utafiti huo wa janga la UVIKO-19 ili kubaini athari zake. Alisema bado wanaendelea na utafiti kupitia wagonjwa wanao waona. Dk. Osati ambaye ni Rais mstaafu wa Chama cha Madaktari Tanzania (MAT), alisema utafiti huo umelenga kuangalia madhara ya muda mrefu yanayotokana na UVIKO-19. "Tunaangalia ubora wa maisha ya watu waliougua kwa kuangalia imewaathiri kwa kiasi gani? Tunaangalia pia gharama za matibabu kwa mgonjwa mmoja mmoja hususani wale waliopata UVIKO-19 kali zaidi," alisema.

Katika ripoti maalum ya mwaka jana pamoja na mambo mengine Dk. Osati alisema ana anafanya utafiti huo ili kubaini athari zake.

Alisema kuwa alikuwa anafanya utafiti kwenye Kifua Kikuu (TB), moyo na mapafu, lakini kupitia Shahada ya Uzamivu (PhD), anayochukua utafiti wake unalenga kuangalia madhara ya muda mrefu ya ugonjwa huo huku akibainisha mpaka wakati huo yalionyesha ni makubwa.

"Utafiti umeonyesha wagonjwa waliopata UVIKO-19 mkali wanapata kitu kinaitwa pafu kutengeneza kovu. Kwa sababu wadudu wanapoingia mwilini kupitia kwenye pua, baadaye kukimbilia kwenye mapafu, yanakuwa ni uwanja wa mapambano kati ya mdudu na kinga za mwili, mapafu yametengenezwa na mifumo midogo midogo inayobeba hewa," alifafanua atika ripoti hiyo. Virusi vipya vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa UVIKO -19, viligunduliwa Novemba mwaka 2019 huko Wuhan, China na kwa Bara la Afrika mgonjwa wa kwanza raia wa kigeni alidungulika Misri.

Machi 16, mwaka jana, Tanzania ilithibitisha mgonjwa wa kwanza wa UVIKO-19, jijini Arusha ambaye aliwasili kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) akitokea Ubelgiji.

Msafiri huyo raia wa Tanzania aliondoka nchini Machi 3, mwaka jana na kati ya Machi 5 na 13, alitembelea nchi za Sweden na Denmark na kurudi tena Ubelgiji.

Siku iliyofuata, Machi 17, mwaka jana, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alitangaza kufunga shule zote za awali, msingi na sekondari hadi kidato cha sita na baadaye vyuo vikuu kwa muda wa siku 30 na baadaye kufunguliwa.

Mpaka sasa waliopata chanjo ya UVIKO -19 ni zaidi ya Watanzania milioni 12 huku uhamasishaji ukiendelea, huku takwimu za vifo na waliougua ugonjwa huo haziko wazi.

# Magugu maji tishio Hifadhi Burunge

**Na Ashton Balaigwa, MANYARA**

JUMUIYA ya Hifadhi ya Wanyamapori Burunge, wilayani Babati mkoani Manyara, imevamiwa na magugu vamizi na kutishia kuharibika kwa ikolojia ya eneo hilo na wanyama wanaokula majani kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Mabadiliko hayo na athari za UVIKO-19, yamesababisha Burunge kupata hasara ya mapato kwa asilimia 40 na kuathiri shughuli zake ikiwamo kuchangia kwenye vijiji vinavyozunguka jumuiya.

Katibu wa jumuiya hiyo, Benson Mwaise, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea hifadhi hiyo kwa lengo la kuangalia juhudi za wananchi kuhifadhi mapito ya wanyama maarufu kama shoroba ya Kwakuchinja na maliasili.

Ziara hiyo ni utekelezaji wa mradi wa Tuhifadhi Maliasili, unafadhiliwa na Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID), unaotekelezwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET).

Alisema magugu vamizi yamesababishwa na mabadiliko ya tabia nchi baada ya mvua zilizonyesha mwaka 2019/2020, ziliambatana na athari mbalimbali kwa wanyama na binadamu. Alifafanua kuwa mimea hiyo imeonekana pembezoni mwa Mto Tarangire na imewatia mashaka kwa kutokujua hatima yake kwenye ikolojia ya wanyamapori na kulazimika kutoa taarifa kwa Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI), kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa kina ili kama itaweza kuleta athari.

Mwaise alitaja athari nyingine za mabadiliko ya tabianchi kuwa ni pamoja na kuharibika kwa miundombinu ya barabara na madaraja na kuathiri utalii wa picha katika eneo la kupokelea wageni hatua ambayo inawalazimu kujenga eneo lingine.

Aidha, alisema madhara ya mvua yamewahamisha wananchi wa eneo kutoka kwenye kilimo na kuingia kwenye uvuvi hatua iliyosababisha kuingia kwa wananchi wasio waadilifu na kushiriki vitendo vya ujangili.

Awali, Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Hamis Juma, alisema kutokana na mazao hayo kuharibiwa na wanyamapori, kumesababisha wakulima kukosa kazi za kufanya na kuhamia kwenye shughuli za uwindaji haramu wa wanyamapori na uvuvi kwa ajili ya kujipatia kitoweo cha kila siku huku wakiasili shughuli za utalii.

Mwenyekiti huyo alisema athari nyingine ni kutokea kwa upungufu wa maji katika mabwawa yanayotumiwa na viboko ambayo yana tope na kuathiri wanyama kiikolojia.

Alisema wanyamapori wengine walio athirika ni wale wanaotegemea kuishi kwa kula wanyama wenzao wakiwamo simba ambao walihamia kula mifugo inayofugwa na kusababisha hasara kwa wananchi. "Kuna mzee mmoja ambaye ng'ombe wake sita waliliwa na simba, jambo lililoongeza hofu kwa jamii kutokana na vitendo vya wanyama hao wakali," alisema Mwaise.

Naye Mkurugenzi wa JET, John Chikomo, alisema mradi wa Tuhifadhi Maliasili umekusudia kutatua changamoto zinazokabili baadhi ya hifadhi kwa waandishi kuandika taarifa sahihi ikiwa ni juhudi za kuunga mkono masuala ya uhifadhi wanyamapori na utalii nchini.


International Commercial Bank (Tanzania) Limited.

**DISCLOSURE MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATION, 2014**

**MINIMUM DISCLOSURE OF BANK CHARGES AND FEES**

| Type of Charge | Item / Transaction | TZS | USD | EURO | GBP |
|---|---|---|---|---|---|
| Minimum Opening Balance | ICB Savings Account | 20,000 | 50 | 50 | 50 |
| | ICB Salary Account | - | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Chuo (Students) Account | 2,000 | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Wazee ( Senior Citizen) Account | Free | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Current Account -Personal | 50,000 | 50 | 50 | 50 |
| | ICB Premier Current Account | 1,000,000 | 500 | 500 | 500 |
| | ICB Premier Savings Account | 1,000,000 | 500 | 500 | 500 |
| | ICB Current Account - Corporate | 100,000 | 100 | 100 | 100 |
| | ICB Lenga (Goal ) Account | 20,000 | 100 | 100 | 100 |
| | ICB Kikundi ( Group ) Account | 50,000 | N/A | N/A | N/A |
| | Al-Wadiyah Savings Accounts | 20,000 | N/A | N/A | N/A |
| Monthly Maintenance Fee | ICB Savings Account | 2,000 | 1.5 | 1.5 | 1.5 |
| | ICB Salary Account | 2,000 | N/A | N/A | N/A |
| | Al-Wadiyah Savings Account | Free | Free | Free | Free |
| | ICB Lenga (Goal ) Account | Free | Free | Free | Free |
| | ICB Kikundi ( Group ) Account | Free | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Wazee (Senior Citizen) Account | Free | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Premier Savings Account | 20,000 | 10 | 15 | 15 |
| | ICB Chuo (Students) Account | Free | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Premier Current Account | 20,000 | 10 | 15 | 15 |
| | ICB Current Account - Corporate | 15,000 | 7 | 7 | 7 |
| | ICB Current Account -Personal | 10,000 | 5 | 5 | 5 |
| Minimum Operating Balance | ICB Savings Account | 5,000 | 100 | 100 | 100 |
| | ICB Salary Account | 5,000 | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Chuo (Students) Account | - | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Wazee ( Senior Citizen) Account | - | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Current Account -Personal | 50,000 | 0 | 0 | 0 |
| | ICB Premier Current Account | 1,000,000 | 500 | 500 | 500 |
| | ICB Premier Savings Account | 500,000 | 500 | 500 | 500 |
| | ICB Current Account - Corporate | 50,000 | 0 | 0 | 0 |
| | ICB Lenga (Goal ) Account | 20,000 | 100 | 100 | 100 |
| | ICB Kikundi ( Group ) Account | 50,000 | N/A | N/A | N/A |
| | Al-Wadiyah Savings Accounts | 5,000 | N/A | N/A | N/A |
| Extra Charge on Transaction below Minimum Balance | ICB Savings Account | 600 | 1.2 | 1.2 | 1.2 |
| | ICB Salary Account | 600 | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Chuo (Students) Account | N/A | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Wazee ( Senior Citizen) Account | N/A | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Staff Savings Account | N/A | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Current Account -Personal | 600 | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Premier Current Account | 5,000 | 1.2 | 1.2 | 1.2 |
| | ICB Premier Savings Account | 5,000 | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Current Account - Corporate | 5,000 | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Lenga (Goal ) Account | 2,000 | N/A | N/A | N/A |
| | Al-Wadiyah Savings Accounts | N/A | N/A | N/A | N/A |
| Cash Withdrawal Fees | Cash withdraw at the counter (All Current accounts): Daily limits | Up to TZS 5Mil - 2000 , Above TZS 5Mil charge 0.13% Max TZS120,000 | 0.25% of the Amount | 0.25% of the Amount | 0.25% of the Amount |
| | Cash withdraw at the counter (All Savings accounts except ICB Chuo and Lenga Account): Daily limits | Up to TZS 5Mil - 1500 , Above TZS 5Mil charge 0.13% Max TZS 170,000 | 0.25% of the Amount | 0.25% of the Amount | 0.25% of the Amount |
| | premature withdrawal and withdrawal more than 1 time per quarter ( ICB Recurring Account & ICB Lenga Account respectively) | 2% charge of the principal amount | 2% charge of the principal amount | 2% charge of the principal amount | 2% charge of the principal amount |
| Fund Transfers / Remittances | Internal Transfers within ICB Bank | Free | Free | Free | Free |
| | Cross border transfers (TT, SWIFT) - outward | N/A | Up to USD50,000.00 charge is USD50 | | |
| | Cross border transfers (TT, SWIFT) - outward | N/A | above USD50,000.00 charge is USD75 | | |
| | Inward Transfers (TT, SWIFT) | Free | USD 15 | | |
| | Amendment of TISS, SWIFT Message | 11,800 | USD 11.8 | | |
| | Amendment of TT, SWIFT Message | N/A | USD 20 | | |
| | TISS | 11,800 | USD 11.8 | | |
| | EFT (Bulk Payments): Out&Inward/salary processing fee | 3,000 per transaction | USD 2 per transaction | | |
| | Stop Payments (TISS/EFT/SWIFT) | 20,000 | USD 20 | | |
| Cash Deposit | ICB Accounts | Free | Free | Free | Free |
| | ICB Agency Banking | Free | N/A | N/A | N/A |
| | Bulk Cash | Free | Free | Free | Free |
| | Deposit of Coins | 0.1% of the Amount | N/A | N/A | N/A |
| | Small Denomination (1, 5, 10, and 20) | N/A | 5% of the Amount | 5% of the Amount | 5% of the Amount |
| Balance Enquiry / Statement | ICB ATM Balance Enquiry | 300 | N/A | N/A | N/A |
| | Balance Enquiry - POS | 300 | N/A | N/A | N/A |
| | Balance Enquiry Within Banking Hall | Free | Free | Free | Free |
| | ICB Internet Banking | Free | Free | Free | Free |
| | ICB Agency Banking | 500 | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Mobile (APP) | Free | Free | Free | Free |
| | interim statement | 1000 per page | 1 per page | 1 per page | 1 per page |
| | Monthly statement & E-statement | Free | Free | Free | Free |
| Cheque Deposit | Cheque From other Banks | Free | Free | Free | Free |
| | Outward Special Clearance – Local Settlement | 53,100 | 52.8 | 46 | 39.5 |
| | Inward Clearing | 1,000 | 1 | 1 | 1 |
| | Inward /Outward cheque return ( technical reason) | 10,000 | 10 | 10 | 10 |
| | Inward /Outward cheque return ( insuffient fund) | 50,000 | 20 | 20 | 20 |
| Cheque Book | Cheque Book 100 Leaves | 100,000 | 50 | 50 | 50 |
| | Cheque Book 50 Leaves | 50,000 | 25 | 25 | 25 |
| | Stop payment order per leaf; Reported Lost/Stolen Cheque Book | 35,000 | 23.6 | 17.7 | 17.7 |
| Bankers Cheque | Commission per issued Cheque | 30,000 | 23.6 | 17.7 | 17.7 |
| | Cancellation of Banker's cheque | 30,000 | 23.6 | 17.7 | 17.7 |
| Standing Instruction | SI - Set up/Amendment/closure | Free | Free | Free | Free |
| | SI-Execution per Entry within ICB | Free | Free | Free | Free |
| | SI-Execution per Entry outside ICB | 20,000 | 10 | 10 | 10 |
| | Unpaid SI due to Insufficient funds | Free | Free | Free | Free |
| ATM /DEBIT CARDS | **ATM Card issuance fee** | | | | |
| | ICB Master Debit Card | 15,000 | 7 | 7 | 7 |
| | ICB Virtual Master Card | 3,400 | 1 | 1 | 1 |
| | Umoja Switch Card | 11,800 | N/A | N/A | N/A |
| | **ATM Card replacement fee** | | | | |
| | ICB Master Debit Card | 16,000 | 7 | 7 | 7 |
| | ICB Virtual Master Card | 3,500 | 1 | 1 | 1 |
| | Umoja Switch Card | 11,800 | N/A | N/A | N/A |
| | **Annual Card Maintenance** | | | | |
| | ICB Master Debit Card | 9,500 | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Virtual Master Card | 35,000 | N/A | N/A | N/A |
| | Umoja Switch Card | 11,800 | N/A | N/A | N/A |
| | **ATM Transaction fee** | | | | |
| | ATM card activation | Free | | | |
| | Blocking/Hotting ATM card | Free | | | |
| | Umoja ATM Cash Withdrawal | 1,300 | N/A | N/A | N/A |
| | Umoja ATM Interbank Fund Transfer | 1,300 | N/A | N/A | N/A |
| | Umoja ATM Intrabank Fund Transfer | 1,300 | N/A | N/A | N/A |
| | Umoja ATM Transfers to Card-Less - (Remmitances) | 1,300 | N/A | N/A | N/A |
| | Umoja ATM Balance Inquiry | 300 | N/A | N/A | N/A |
| | Umoja ATM Mini Statement | 300 | N/A | N/A | N/A |
| | POS Withdrawal up to TZS 20,000,000 | 2,000 | N/A | N/A | N/A |
| | ATM Cash Withdrawal fee per transaction Mastercard local | 4,000 | Local trn < USD15 0.5%: Local trn >USD15 - 1.1% : Cross- border 1.6% | | |
| | ATM Cash Withdrawal fee per transaction Mastercard International | 8,000 | | | |
| Internet / Mobile Banking | Registration | Free | Free | | |
| | Monthly Service Fee (Corporate) | 15,000 | USD 8 | | |
| | Monthly Service Fee (Personal) | 7,000 | USD 4 | | |
| | Funds Transfer between Selcom managed banks | TZS 500 | | | |
| | Funds Transfer from Bank account to agents | TZS 500 | | | |
| | NHC payments | TZS 1,000 | | | |
| | Selcom Card funds transfers | TZS 500 | | | |
| | TANESCO Postpaid Electricity Bill payment | Free | | | |
| | TFDA- Certification application fee payment | TZS 1,000 | | | |
| | Transfers through ICB Internet Banking | TZS 1,000 | | | |
| | Transfers through Internet Banking File Upload Within | TZS 500 | | | |
| | Transfers through Internet Banking File Upload TISS | TZS 5,000 | | | |
| | Transfers through Internet Banking File Upload EFT | TZS 1,000 | | | |
| | Transfers through Internet Banking File Upload B2W | TZS 500 | | | |
| | UTT investor payments | TZS 1,000 | | | |
| | DSTV Payments | | | | |
| | 1 - 200,000/- | TZS 1,000 | | | |
| | 200,000.01 to 500,000 | TZS 2,000 | | | |
| | 500,000.01 + | TZS 5,000 | | | |
| Electronic Money Transaction Levy - All withdrawals over the counters, ATM, and transfers (local and abroad) | **Electronic Money Transactions amount in TZS** | Rate in TZS | | | |
| | 100 to 2,999 | 10 | Equivalent to TZS | Equivalent to TZS | Equivalent to TZS |
| | 3,000 to 3,999 | 15 | | | |
| | 4,000 to 4,999 | 30 | | | |
| | 5,000 to 6,999 | 60 | | | |
| | 7,000 to 9,999 | 70 | | | |
| | 10,000 to 14,999 | 128 | | | |
| | 15,000 to 19,999 | 243 | | | |
| | 20,000 to 29,999 | 383 | | | |
| | 30,000 to 39,999 | 439 | | | |
| | 40,000 to 49,999 | 599 | | | |
| | 50,000 to 99,999 | 818 | | | |
| | 100,000 to 199,999 | 1,009 | | | |
| | 200,000 to 299,999 | 1,173 | | | |
| | 300,000 to 399,999 | 1,397 | | | |
| | 400,000 to 499,999 | 1,636 | | | |
| | 500,000 to 599,999 | 2,075 | | | |
| | 600,000 to 699,999 | 2,554 | | | |
| | 700,000 to 799,999 | 2,833 | | | |
| | 800,000 to 899,999 | 3,000 | | | |
| | 900,000 to 1,000,000 | 3,551 | | | |
| | 1,000,001 to 3,000,000 | 3,751 | | | |
| | 3,000,001 and above | 4,000 | | | |
| General Account Operations | Confirmation of Balance and Audit Statement | 50,000 | 25 | 25 | 25 |
| | Salary processing manually per entry | 500 | N/A | N/A | N/A |
| | Salary and Bulk payments outside the Bank | 3,000/transaction plus transfer fee | N/A | N/A | N/A |
| | Advisory service - charged per advice | 2,500 | Equivalent to TZS | Equivalent to TZS | Equivalent to TZS |
| | Vouchers - Information less than one year | 15,000 | Equivalent to TZS | Equivalent to TZS | Equivalent to TZS |
| | Salary Alert per message | 118 | N/A | N/A | N/A |
| | Court Order Closing of Account | Free | Free | Free | Free |
| | Deliberate closing of Corporate account | 20,000 | 10 | 10 | 10 |
| | Deliberate closing of Personal account | 11,800 | 5 | 5 | 5 |
| | **Cash Change** | | | | |
| | Cash Coins per bag of TZS 100,000 | 1,180 | N/A | N/A | N/A |
| Bonds & Guarantee | Issuance of Bid Bond - Cash cover | 0.5% per Quarter | | | |
| | Issuance of Bid Bond - Other Security | 1.42% Per Quarter | | | |
| | Perfomance Bond-Cash Cover | 0.5% per Quarter | | | |
| | Perfomance Bond-Other security | 1.42% Per Quarter | | | |
| | Extentions | 1.42% Per Quarter | | | |
| | Amendments | Simple amendments$50 | | | |
| | Cancellations of Returned guarantees | Free | | | |
| | Cancellations of guarantees if not Returned | 20000 | | | |
| Advanced Payment Guarantee | Issuance - Cash cover | 0.5% Min 100,000 | | | |
| | Issuance - Security | 1.42% Min100,000 | | | |
| | **Import Collections (IC)-Inward Foreign Doc & Bills for Collections** | | | | |
| | Handling Commissions | 0.5% Min usd 100 | | | |
| | Correspondance swift charges | Usd 50 | | | |
| | **Export Collections (EC)-Outwar Foreign Doc & Bills for Collections** | | | | |
| | Handling Commissions | 0.5% Min usd 100 | | | |
| | Correspondance Commission-per tracer | Usd 50 | | | |
| | Courier Charges | Usd 100 | | | |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

**Name:**

Sanjeev Anand — Chief Executive Officer — 26.07.2022

Francisco Mwageni — Ag: Head of Marketing — 26.07.2022

John Mwakasonda — Head of Internal Audit — 26.07.2022

# Makarani sensa watakiwa uvumilivu wakati wa kuhesabu

**Na Thobias Mwanakatwe, SINGIDA**

MKUU wa Mkoa wa Singida, Dk. Binilith Mahenge, amewataka wakufunzi wa sensa mkoani hapo waliohitimu mafunzo ya ukarani kuwa wavumilivu katika utekelezaji wa kazi hiyo ili kupata taarifa na takwimu sahihi ambazo zitasaidia serikali kupanga maendeleo ya wananchi wa mkoa huo.

Alisema hayo jana wakati akifunga mafunzo ya wakufunzi wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 yaliyokuwa yakifanyika mjini hapo yaliyodumu kwa siku 21.

Dk. Mahenge alisema zitajitokeza changamoto ndogo ndogo wakati wa utekelezaji wa kazi hiyo ikiwamo mtu kutokuwa na haraka ya kujieleza au ucheleweshaji wa muda, karani asije akaweka data za uongo ili kuokoa muda kwa sababu itakuwa ni hasara kwa taifa.

"Isije ikatokea kwa namna yoyote karani akatengeneza taarifa ili mradi awahi kwenda kwenye kaya nyingine, hatutahitaji data za kupika, serikali imejitoa kuhakikisha mnapata mafunzo na mmepatiwa vitendea kazi "vishikwambi," alisema.

Hata hivyo, aliwapongeza wakaguzi hao kwa ufaulu huku akiwaambia watumie bahati waliyoipata kuisaidia serikali kufikia malengo yake.

Mkuu wa Wilaya ya Singida, Mhandisi Paskasi Muragili alisema kwa mafunzo yaliyotolewa hawategemei jambo lolote kuharibika kwa kuwa pamoja na masomo ya darasani, wakufunzi hao walijifunza kwa vitendo vijijini.

Aliwataka kwenda kuwafundisha wengine katika ngazi ya wilaya kama ilivyofanyika kwao ili kuhakikisha hawapotezi maana halisi iliyopangwa.

Kwa upande wake, Mratibu wa Sensa Mkoa wa Singida, Naing'oya Kipuyo, akitoa taarifa ya mafunzo hayo alisema wahitimu hao wamefaulu kwa asilimia 70 ambapo walipata elimu ya matumizi ya madodoso manne.

Madodoso hayo ni pamoja na makundi maalum, ambalo linahusu ukusanyaji wa taarifa za makundi ambayo hayawezi kuhesabiwa na madodoso ya kawaida.

Kipuyo alisema wakufunzi hao wapatao 215 wanatarajia kwenda kuwafundisha makarani ambao ndiyo watakuotumika katika kuhesabu watu na makazi.

Naye Neema Luphebia, Mkurugenzi wa Sensa Mkoa wa Singida, ameiomba jamii kuhakikisha wanajitokeza kuhesabiwa kwa kuwa ni zoezi ambalo halichukui muda mrefu na lina usiri mkubwa.

# Mita janja kuanza kuunganishiwa wateja Septemba

**Na Gurian Adolf, SUMBAWANGA**

SERIKALI imesema kuanzia mwezi Septemba itaanza kuwaunganishia umeme wateja wapya kwa kutumia Mita Janja ili mkusaidia kununua umeme akiwa safarini bila kulazimika kuingiza kwenye mita yake.

Waziri wa Nishati, Januari Makamba, ameyasema hayo jana wakati akijibu swali kwa mmoja wa wananchi wa mkoa huo aliyetaka kujua ni lini Shirika la Umeme nchini (TANESCO) litaanza kuwafungia wateja wake mita za aina hiyo kwa kuwa baadhi yao wanazisubiri kwa hamu kubwa.

Waziri Makamba, alizungumza na wakazi wa mkoa huo na kutoa ufafanuzi mambo mbalimbali ya wizara yake kupitia kituo kimoja cha redio cha mkoani humo wakati akiwa katika ziara ya kikazi ya siku moja mkoani Rukwa.

Alisema Wizara ya Nishati kupitia TANESCO, ilitangaza kuanzia mwezi Julai, mwaka huu ingeanza kuwaunganishia umeme wateja wapya kwa kutumia Mita Janja (Smart Meter), lakini kutokana na taratibu za ununuzi kutokamilika kwa wakati ilishindikana kuanza mwezi huo.

Makamba alisema tayari TANESCO imempata mzabuni na imekubaliana naye ataingiza mita hizo mpya zipatazo 300,000 ambazo zitatumika kuwaunganishia umeme wateja wapya kuanzia mwezi Septemba na wateja wa zamani wataendelea kubadilishiwa mita zao taratibu.

Waziri Makamba pia aliwataka wananchi wanaoishi kwenye vitongoji nchini kuwa wavumilivu kwa kuwa kuanzia mwezi Januari 2023, serikali itaanza kuunganisha umeme kwa wananchi walioko kwenye vitongoji vyote vilivyoko nchini, mpango wa mwanzo ilikuwa kuunganisha umeme kwenye vijiji vyote nchini.

Awali, akiwa katika kisiwa cha Mandakelenge, Ziwa Tanganyika, wilayani Nkasi, Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kaskazini, Aidan Khenani, alimwomba waziri kuhakikisha wananchi walioko katika visiwa vya ziwa hilo wanapata nishati ya umeme pamoja na gesi.

Alisema wakazi wa visiwa hivyo wanahangaika kupata nishati ya kupikia kwa kuwa wamekata miti kwa ajili ya kuni na kuchoma mkaa na hawana nishati mbadala na kusababisha maeneo yao kuanza kugeuka jangwa na kuwalazimu kusafiri kwa mitumbwi umbali mrefu ili kutafuta kuni, hali inayohatarisha maisha yao.

Khenani alisema, wajasiriamali walioko katika visiwa vya Mandakelenge, Manda Ulwile, Mvuna pamoja na Kalungu wengi wao ni wanawake wanaofanya biashara za kuuza samaki wa kukaanga na wateja wao wanatoka mataifa ya Rwanda, Burundi na Zambia, kama wakipata nishati ya umeme na gesi itawasaidia kufanya shughuli zao katika mazingira salama.



Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Singida, Mhandisi Florence Mwakasege, akizungumza na wananchi wa Kata ya Iguguno wilayani Mkalama juzi, wakati akisikiliza mahitaji na ushauri wao kuhusu sekta ya nishati. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# IMC yashinda tuzo ya ubora ubunifu

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Imperial Marketing and Communications (IMC), imeshinda tuzo bora ya ubunifu kwa mwaka huu wakati wa tuzo za Tanzania Marketers Awards zilizoandaliwa na Chama cha Sayansi na Masoko Tanzania (Tanzania Marketing Science Association - TMSA).

Akizungumza jijini Dar es Salaam baada ya kupokea tuzo hiyo, Mkurugenzi Mtendaji Imperial Marketing and Communications (IMC), Murtaza Ebrahim, alisema kampuni hiyo inajihusisha na uwakala yenye uzoefu kwenye huduma jumuishi.

"Tunayo furaha kupata tuzo hii katika soko la ushindani na inaonyesha dhamira yetu katika kubadilisha jinsi biashara inavyoshirikiana na wateja na kuhakikisha wanakuwa na uwezo wa kujiendeleza kwa kupitia bidhaa na huduma zao kupitia ubunifu, alisema Murtaza na kuongeza:

"Tunashukuru sana wateja wetu ambao wametuamini na kutupa fursa ya kuhama kutoka dhana ya zamani na kukubali dhana mpya ya 'Phygital' ambayo ni dhana ya kidijitali kwa kutumia teknolojia shirikishi, ili kukuza biashara na masoko kwa kutumia teknolojia bunifu."

Murtaza aliongeza: "Tuzo hii ya ubunifu ni uthibitisho kuwa kampuni yetu ni bora kwenye suluhisho la ubunifu ambazo zinawanufaisha wateja na tutaendelea kutafuta njia mpya za kuendelea kuboresha huduma zetu kwa manufaa ya wateja ambao tunawahudumia."

Alisema: "Tuzo hii sio kwa IMC pekee mbali pia kwa wateja ambao wamechangia sehemu kubwa kufanikisha hili kwa kutupa fursa ya kuonyesha uwezo wetu wa ubunifu. Tutaendelea kujituma ili kuleta ushindani kwenye soko la ubunifu ambalo linazidi kukua siku hadi siku."

ama
ALHAMISI JULAI 28, 2022
AFYA NA MAZINGIRA

ZIARA YA SIKU TATU DK PHILIP MPANGO MKOA KATAVI



Ukurasa 14



Ukurasa 14

...Mimba za utotoni 45%, udumavu 35% zamchefua, awaachia angalizo 'hili hapana'

AFYA

# Ugonjwa wa kisukari ulivyo chanzo kikubwa mikasa ya upofu duniani

• Kuzuia ni hatua ya tahadhari inayosisitizwa kote

**Na Dk. Rajabu Mlaluluko**

KISUKARI kinatajwa ni ugonjwa unaotokana na kiwango cha sukari kwenye damu kuwa juu, kutokana na kongosho kushindwa kuzalisha kiwango cha homoni ya Insulin au kushindwa homoni ya Insulin haifanyi kazi vizuri kwenye misuli na ini (Insulin insensitivity).

Hiyo inatokana na kubadilika kwa mitindo ya maisha; kutokufanya mazoezi na ulaji mbaya wa vyakula kama chipsi na vingine vyenye mafuta mengi, kuchangia kuwapo tatizo la magonjwa yasiyoambukiza kama Kisukari kuongezeka duniani na Tanzania kwa ujumla.

Inakadiriwa kuwa ongezeko hadi kufika mwaka 2030, asilimia 46 ya vifo Kusini mwa Jangwa la Sahara, vitatokana na magonjwa yasiyoambukiza kama kisukari na shinikizo la damu.

Vivyo hivyo, itakapofika mwaka 2040, kunakaridiwa watu milioni 442 duniani watakuwa wana ugonjwa wa kisukari, huku watu milioni 224 wakiwa na madhara yanayotokana na kisukari kwenye macho (diabetic retinopathy). Hiyo inaenda na matarajio ya watu milioni 70 watapata madhara makubwa yatakayowapa upofu.

Kwa Tanzania, kuna idadi asilimia 12.3 ya watu wote wenye umri kati ya miaka 20 na 79 walikuwa na ugonjwa huo mwaka jana.

Kwa kutumia uzoefu katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, kisukari ni ugonjwa hatari sana kwa afya ya mwanadamu, kwani unaweza kuathiri nyenzo zote za mwili zikiwepo macho, moyo, mishipa midogo ya damu, mishipa ya fahamu, figo na mfumo wa kinga ya mwili.



Mlo wa mgonjwa wa kisukari.



Tabibu akimhudumia mgonjwa kisukari. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Ni namna inayojenga haja ya kuzingatiwa jamii kupima na kufuata matibabu kwa watakaogundulika. Msingi uliopo, kisukari kwenye macho kinatajwa kuathiri mishipa midogo ya damu kwenye pazia la ndani (retina) kwa kuharibu na kufanya kuzalishwe kemikali inayofanya kutengenezwa mishipa mipya ya damu, ambayo huwa ni dhaifu na rahisi kupasuka, hata kusababisha upofu wa ghafla kutokana na damu kuvuja ndani ya jicho.

Vivyo hivyo, hali ya kisukari inaweza kusababisha kupitia kuwapo mtoto wa jicho kwa mgonjwa maarufu 'diabetic cataract'. Hapo kunatajwa baadhi ya vitu vinavyoibua madhara hayo kwenye macho kuwa makubwa na kwa haraka.

> **Kwa Tanzania, kuna idadi asilimia 12.3 ya watu wote wenye umri kati ya miaka 20 na 79 walikuwa na ugonjwa huo mwaka jana.**

Kunatajwa sababu zilizopo ni: Mgonjwa wa kisukari kushindwa kuthibiti kiwango cha sukari kwenye damu, ugonjwa wa shinikizo la damu, kiwango kikubwa cha mafuta mabaya kwenye damu na ujauzito, hata kujenga sababu za kitaalamu, mwanamke mwenye kisukari, anahimizwa kuonwa na mtaalamu wa macho kabla na baada ya kupata ujauzito.

Ushauri mkuu ulioko ni kwamba: "Watu wajitahidi kuepuka vyakula vya mafuta mengi, wajitahidi kufanya mazoezi. Wagonjwa wa kisukari wajitahidi kufuata ushauri wa wataalamu wa afya kwa kutumia dawa vizuri na kuhakikisha wanaonana na wataalamu wa macho, ili kuchunguzwa madhara ya kisukari kwenye macho yao hata kama hawajaanza kuona dalili yoyote."

**Mwandishi, ni bingwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya. Anapatikana kwa barua pepe: drrajabumlaluko@gmail.com na simu; +255 753 93 86 28**

NMB
Karibu yako

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

# NMB BANK PLC

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | KUNDI | | BENKI | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Robo Mwaka ya sasa 30.06.2022 | Robo Mwaka iliyopita 31.03.2022 | Robo Mwaka ya sasa 30.06.2022 | Robo Mwaka iliyopita 31.03.2022 |
| **A.** | **MALI** | | | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 456,104 | 411,405 | 456,104 | 411,405 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 921,204 | 886,237 | 921,204 | 886,237 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 1,908,939 | 1,886,692 | 1,908,939 | 1,886,692 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 315,724 | 484,403 | 315,724 | 484,403 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 4,286 | 16,493 | 4,286 | 16,493 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | 1,535 | - | 1,535 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 12,933 | 13,741 | 12,933 | 13,741 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 5,033,458 | 4,791,729 | 5,033,458 | 4,791,729 |
| 12 | Mali Nyingine | 214,088 | 202,355 | 245,071 | 233,121 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 2,920 | 2,920 | 42,558 | 42,558 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 181,374 | 187,105 | 150,538 | 155,761 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **9,051,030** | **8,884,615** | **9,090,815** | **8,923,675** |
| **B.** | **DHIMA** | | | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 20,305 | 53,141 | 20,305 | 53,141 |
| 18 | Amana za Wateja | 6,578,726 | 6,568,063 | 6,584,272 | 6,569,222 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 260,603 | 84,426 | 260,603 | 84,426 |
| 20 | Amana Maalumu | 10,985 | 61,564 | 10,985 | 61,564 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 2,155 | 2,168 | 2,155 | 2,168 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 79,395 | 66,117 | 82,212 | 68,716 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 1,036 | - | 1,036 | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadaye | 45,456 | 43,674 | 45,456 | 43,674 |
| 27 | Dhima Nyingine | 82,867 | 72,737 | 119,019 | 111,969 |
| 28 | Madeni | 494,160 | 476,389 | 494,160 | 476,389 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **7,575,688** | **7,428,279** | **7,620,203** | **7,471,269** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **1,475,342** | **1,456,336** | **1,470,612** | **1,452,406** |

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | KUNDI | | BENKI | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Robo Mwaka ya sasa 30.06.2022 | Robo Mwaka iliyopita 31.03.2022 | Robo Mwaka ya sasa 30.06.2022 | Robo Mwaka iliyopita 31.03.2022 |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 1,233,290 | 1,330,019 | 1,234,099 | 1,330,828 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 207,839 | 101,216 | 206,283 | 100,460 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 10,230 | 1,118 | 10,230 | 1,118 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 3,983 | 3,983 | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **1,475,342** | **1,456,336** | **1,470,612** | **1,452,406** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 1,569,415 | 1,366,006 | 1,569,415 | 1,366,006 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 196,465 | 186,182 | 196,465 | 186,182 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 202,235 | 201,112 | 202,235 | 201,112 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 3,590 | 3,453 | 3,590 | 3,453 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 16% | 16% | 16% | 16% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 3.8% | 3.7% | 3.8% | 3.7% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 76% | 74% | 76% | 74% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 56% | 54% | 55% | 54% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 80% | 81% | 80% | 81% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 2% | 2% | 2% | 2% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 2% | 2% | 2% | 2% |

Trilioni 9
Jumla ya Mali
+19% YoY

Trilioni 6.6
Amana za Wateja
+13% YoY

Trilioni 5
Mikopo Halisi Iliyopo
+19% YoY

3.8% Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | KUNDI | | BENKI | | KUNDI | | BENKI | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Robo ya Mwaka sasa 30.06.22 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30.06.21 | Robo ya Mwaka sasa 30.06.22 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30.06.21 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30.06.22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30.06.21 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30.06.22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30.06.21 |
| 1 | Mapato ya Riba | 229,771 | 196,030 | 229,771 | 196,030 | 453,673 | 386,799 | 453,673 | 386,799 |
| 2 | Gharama za Riba | (39,628) | (30,497) | (39,628) | (30,497) | (76,268) | (63,356) | (76,268) | (63,356) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **190,143** | **165,533** | **190,143** | **165,533** | **377,405** | **323,443** | **377,405** | **323,443** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (17,016) | (30,169) | (17,016) | (30,169) | (31,060) | (53,039) | (31,060) | (53,039) |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **97,572** | **74,228** | **97,572** | **74,228** | **184,891** | **139,915** | **184,891** | **139,915** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 10,664 | 7,293 | 10,664 | 7,293 | 20,896 | 12,867 | 20,896 | 12,867 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 76,158 | 60,166 | 76,158 | 60,166 | 148,025 | 115,987 | 148,025 | 115,987 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 10,750 | 6,769 | 10,750 | 6,769 | 15,970 | 11,061 | 15,970 | 11,061 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(117,671)** | **(109,339)** | **(118,678)** | **(110,500)** | **(233,128)** | **(216,373)** | **(235,097)** | **(218,236)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (65,524) | (57,127) | (65,524) | (57,127) | (130,188) | (113,590) | (130,188) | (113,590) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (3,509) | (3,613) | (3,509) | (3,613) | (6,923) | (7,161) | (6,923) | (7,161) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (48,638) | (48,599) | (49,645) | (49,760) | (96,017) | (95,622) | (97,986) | (97,485) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **153,028** | **100,253** | **152,021** | **99,092** | **298,108** | **193,946** | **296,139** | **192,083** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (46,405) | (30,137) | (46,197) | (30,137) | (90,269) | (58,443) | (89,856) | (58,443) |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **106,623** | **70,116** | **105,824** | **68,955** | **207,839** | **135,503** | **206,283** | **133,640** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa Faida/(Hasara) uthamanishaji Dhamana za Kuuzwa | 9,112 | 62 | 9,112 | 62 | 9,666 | (272) | 9,666 | (272) |
| | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **115,735** | **70,178** | **114,936** | **69,017** | **217,505** | **135,231** | **215,949** | **133,368** |

| | | KUNDI | | BENKI | | KUNDI | | BENKI | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Robo ya Mwaka sasa 30.06.22 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30.06.21 | Robo ya Mwaka sasa 30.06.22 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30.06.21 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30.06.22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30.06.21 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30.06.22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30.06.21 |
| 12 | Idadi ya Waajiriwa | 3,518 | 3,473 | 3,518 | 3,473 | 3,518 | 3,473 | 3,518 | 3,473 |
| 13 | Mapato kwa Hisa | 213 | 140 | 212 | 138 | 416 | 271 | 413 | 267 |
| 14 | Idadi ya Matawi | 227 | 225 | 227 | 225 | 227 | 225 | 227 | 225 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Mali | 5% | 4% | 5% | 4% | 5% | 4% | 5% | 4% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 29% | 23% | 28% | 23% | 28% | 23% | 28% | 22% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 41% | 46% | 41% | 46% | 41% | 47% | 42% | 47% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 10% | 11% | 11% | 12% | 10% | 11% | 11% | 12% |

Bilioni 298
Faida kabla ya Kodi ya Mapato
+54% YoY

Bilioni 208
Faida Baada ya Kodi ya Mapato
+53% YoY

Uwiano wa Matumizi yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi
42%

216963802

*YoY - Linganishi mwaka kwa mwaka

www.nmbbank.co.tz

**NMB**
Karibu yako

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

# NMB BANK PLC

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA

### KWA ROBO/ MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | KUNDI | | BENKI | | KUNDI | | BENKI | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Robo Mwaka ya sasa | Robo Mwaka iliyopita | Robo Mwaka ya sasa | Robo Mwaka iliyopita | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
| | 30.06.2022 | 31.03.2022 | 30.06.2022 | 31.03.2022 | 30.06.2022 | 30.06.2021 | 30.06.2022 | 30.06.2021 |
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 153,028 | 145,080 | 152,021 | 144,118 | 298,108 | 193,946 | 296,139 | 192,082 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 2,551 | 6,641 | 2,208 | 6,133 | 9,192 | 19,907 | 8,341 | 18,922 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (240,921) | (151,537) | (240,921) | (151,537) | (392,458) | (168,159) | (392,458) | (168,088) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 103,425 | 103,897 | 107,812 | 103,682 | 207,322 | 536,658 | 211,494 | 538,797 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 26,213 | 15,353 | 23,350 | 14,474 | 41,566 | (31,328) | 37,824 | (26,601) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 2,503 | 43,299 | 2,286 | 45,656 | 45,802 | (8,148) | 47,942 | (12,236) |
| - Kodi Iliyolipwa | (37,933) | (38,097) | (37,890) | (37,890) | (76,030) | (55,911) | (75,780) | (55,911) |
| - Mengineyo (SMR) | 2,095 | (448) | 2,095 | (448) | 1,647 | (22,570) | 1,647 | (22,570) |
| **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **10,961** | **124,188** | **10,961** | **124,188** | **135,149** | **464,395** | **135,149** | **464,395** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (5,292) | (6,626) | (5,292) | (6,626) | (11,918) | (5,675) | (11,918) | (5,675) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo (Uwekezaji katika Hisa na Amana) | (13,135) | (146,857) | (13,135) | (146,857) | (159,992) | (41,565) | (159,992) | (41,565) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(18,427)** | **(153,483)** | **(18,427)** | **(153,483)** | **(171,910)** | **(47,240)** | **(171,910)** | **(47,240)** |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | (96,729) | - | (96,729) | - | (96,729) | (68,500) | (96,729) | (68,500) |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 17,771 | (17,826) | 17,771 | (17,826) | (55) | (70,403) | (55) | (70,403) |
| Mengineyo (Mabadiliko yatokanayo na bei za fedha za kigeni) | - | - | - | - | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **(78,958)** | **(17,826)** | **(78,958)** | **(17,826)** | **(96,784)** | **(138,903)** | **(96,784)** | **(138,903)** |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | | | | | |
| Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (86,424) | (47,121) | (86,424) | (47,121) | (133,545) | 278,252 | (133,545) | 278,252 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 1,359,376 | 1,406,497 | 1,359,376 | 1,406,497 | 1,406,497 | 907,029 | 1,406,497 | 907,029 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **1,272,952** | **1,359,376** | **1,272,952** | **1,359,376** | **1,272,952** | **1,185,281** | **1,272,952** | **1,185,281** |

## TAARIFA YA KUNDI YA MABADILIKO YA MTAJI

### KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Uthamanishaji Amana za Kuuzwa) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2022** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | **-** | **1,330,019** | **-** | **-** | **4,547** | **1,354,566** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 207,839 | - | - | - | 207,839 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 9,666 | 9,666 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (96,729) | - | - | - | (96,729) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | **-** | **1,441,129** | **-** | **-** | **14,213** | **1,475,342** |
| **Mwaka Uliopita 2021** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | **-** | **1,106,441** | **-** | **-** | **4,704** | **1,131,145** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 135,503 | - | - | - | 135,503 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | (272) | (272) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (68,500) | - | - | - | (68,500) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | **-** | **1,173,444** | **-** | **-** | **4,432** | **1,197,876** |

## TAARIFA YA BENKI YA MABADILIKO YA MTAJI

### KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Uthamanishaji Amana za Kuuzwa) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2022** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | **-** | **1,330,828** | **-** | **-** | **564** | **1,351,392** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 206,283 | - | - | - | 206,283 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 9,666 | 9,666 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (96,729) | - | - | - | (96,729) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | **-** | **1,440,382** | **-** | **-** | **10,230** | **1,470,612** |
| **Mwaka Uliopita 2021** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | **-** | **1,109,142** | **-** | **-** | **792** | **1,129,934** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 133,640 | - | - | - | 133,640 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | (272) | (272) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (68,500) | - | - | - | (68,500) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | **-** | **1,174,282** | **-** | **-** | **520** | **1,194,802** |

## BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA JUNI 2022

**Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Ruth Zaipuna<br>**Afisa Mtendaji Mkuu** | | Julai 22, 2022 |
| Juma Kimori<br>**Afisa Mkuu wa Fedha** | | Julai 22, 2022 |
| Benedicto Baragomwa<br>**Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | | Julai 22, 2022 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Dkt. Edwin P. Mhede<br>**Mwenyekiti wa Bodi** | | Julai 22, 2022 |
| Benson Mahenya<br>**Mkurugenzi** | | Julai 22, 2022 |



AFYA

## ZIARA YA DK PHILIP MPANGO KATAVI

# Mimba za utotoni 45%, udumavu 35% zamchefua, awapa angalizo 'hili hapana'

• Aondoka, akimuachia RC maagizo

**Na Neema Hussein,** Mpanda

NI siku chache zilizopita Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, amemaliza ziara ya siku tatu mkoani hapa, Katavi. Ni aina ya ugeni wa kitaifa ambao umeondoka na karipio la kiuzazi nyumbani, hasa akikemea na rekodi asiyokubaliana nayo katika mimba za utotoni, pia udumavu.

Hiyo inakuja ndani muda mfupi nayo ikihesabu siku kadhaa, gazeti Nipashe likichapisha makala mahsusi inayochambua kwa undani mimba za utotoni ilivyo katika hatua isiyoridhisha wilayani Mlele, hata asasi ya Maria Stopes kufunga safari kuutafiti undani wa kasoro hiyo.

Makamu wa Rais Dk. Mpango katika ziara yake hiyo ya siku tatu mkoani Katavi iliyokoma wiki iliyopita, naye akasimamia hoja hiyo, katika halmashauri zote za mkoa huo alizozitembelea na kuzungumza na wananchi, hakuacha kukemea jambo hilo.

Dk. Mpango anasema, mimba za utotoni bado ni changamoto kubwa kitaifa, huku akiutaja mkoa wa Katavi kuongoza kwa tatizo hilo kitaifa kwa asilimia 45, akionyesha kidole cha hali ya kutofurahishwa na hilo.

"Nimeambiwa hapa kwa wastani kila robo mwaka jumla ya watoto wa kike zaidi ya 100 wenye umri kati ya miaka 12 na 16 wanabainika kwamba wamepata mimba za utotoni. Hili hapana!

"Nimefurahishwa sana kwa mambo mengine, lakini hili lazima niseme linasababisha hata vifo vya hawa watoto wanapokwenda kujifungua haiwezekani!" akawaambia wakazi wa Mpanda, huku akiwashangilia 'Mpanda Oyee, Mpanda Oyee!...'

Dk. Mpango akaendelea: "Muwaache watoto wasome elimu oyee,elimu oyeee! Kuna wengine mnaoza watoto wetu mapema mno! Wapeni nafasi ya kusoma ili tupate wasomi huyu mama mzuri huyu kama ndiyo angepata mimba ya utotoni. asingekuwa Naibu Waziri sasa (anatoa mfano wa jukwaani).

"Sasa tumefika mahali Rais wa nchi yetu ni mwanamama. Wapeni nafasi mabinti zetu wasome shule na vyombo vinavyohusika mheshimu. Mkuu wa Mkoa (Mwanamvua Mrindoko) na timu yako watafuteni hao wanaotuharibia watoto wetu wasiendelee na shule.

"Tumeelewa?" anahoji na kuendeleza maagizo" Nataka kusikia 'dropout' (wanaoacha shule) imepungua hao wanaokatiza masomo waishe kabisa katika mkoa wa Katavi. Watoto 4,500 (wanaoacha shule) ni wengi mno. Tunapoteza rasilimali kubwa ya taifa...Katavi oyeee, Katavi oyeee!"anatamka



**PICHA**:Makamu wa Rais,Dk. Philip Mpango wakati alipokuwa ziarani mkoani Katavi,ambapo alikagua na kuzindua miradi mbalimbali ya maendeleo na kuzungumza na wananchi ikiwemo kukabidhi hundi ya shilingi bilioni 2.3 kwa vijiji vilivyo nufaika na biashara ya hewa ukaa.

> **Hapo anawataka viongozi mbalimbali wa dini, serikali na taasisi mbalimbali walivalie njuga suala hilo kwa kuhimiza elimu ya lishe.**



Dk.Mpango.

Ni kauli aliyotoka nayo Mpanda, akahama nayo katika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, anakopewa taarifa na Mkuu wa Mkoa kuhusu tatizo la mimba, nako kunachefua na kukafunguga hisia zake:

"Ndugu zangu wa Tanganyika na mkoa mzima wa Katavi, rasilimali muhimu katika taifa lolote ni rasilimali watu. Ni lazima iwe ni rasilimali yenye ubora, lakini maana yake ni nini?...Maana yake lazima watu wetu wapate elimu, lakini taarifa iliyopo watoto wa wilaya hii, watoto wa mkoa huu baadhi yao hawamalizi shule.

"Kuna ndoa za utotoni, kuna mimba za watoto wa shule ambazo zinawafanya waache shule. Ndugu zangu wa Tanganyika, nawasihi kweli kweli, muwaache watoto wasome. Narudia tena, tuwape nafasi watoto wa kike na kiume wamalize shule!

"Nimefurahi sana nimesimama pale njiani kalikuwepo 'kabinti' kamoja kazuri kweli, kakasema 'mimi nataka kuwa daktari'nikawauliza na wengine wakasema 'mimi nataka kuwa kama Mama Samia' Huwezi kuwa daktari bila kusoma,"akasema Dk. Mpango, ambaye ni msomi mahiri wa uchumi, ngazi ya daktari wa falsafa.

Katika hatua hiyo, akamtaka Mkuu wa Mkoa, Mwanamvua Mrindoko na timu yake ya Ulinzi na Usalama, kutosita kuwachukulia hatua wazazi wanaobainika kutaka kuwaoza watoto kabla ya kumaliza shule.

"Mimba ni tatizo, watoto hawa wanapata fistula wakati wa kujifungua, wengine wanapoteza kabisa maisha. Tusichezeane, lazima tujenge taifa kuna vitu ambavyo tunachekeana, lakini sio kwa hili," akasema Dk.Mpango.

### AJENDA YA UDUMAVU

Ukali wa Dk.Mpango, akionyeha kutotaka masihara nayo ikahamia katika suala la tatizo la udumavu mkoani Katavi, akisema ni tatizo kubwa, licha ya kwamba mkoa wa Katavi unazalisha chakula kwa wingi.

Hapo anaamua kurejea takwimu alizo nazo za utafiti uliofanyika mwaka 2018 kwamba mkoa wa Katavi kwa sasa ni takribani asilimia 35.7 ya watoto wana tatizo la udumavu.

Hapo akawarejesha darasani, akiwaambia kwamba jumla ya siku 1000 tangu mimba ya mtoto inatungwa hadi kuzaliwa ni kipindi muhimu sana katika makuzi ya kibinadamu na ndio maana kunasisitizwa mahudhurio ya kliniki.

"Ndio maana unakuta saa nyingine hata walimu wanawapiga watoto,wewe mbona huelewi kama wenzako? Kumbe walipata lishe duni na wengine wanasema wewe mbona huna kipaji kama wenzako, hata kazini unakuta wengine wana uwezo mdogo wa kupenda kazi, kumbe tatizo ni kile kipindi cha miaka miwili hakupata lishe bora.

"Nimeshtushwa sana na takwimu ambazo zinaonyesha mkoa wa Katavi ni kati ya mikoa ambayo ina tatizo la watoto wenye udumavu na takwimu hizo ndio zinaongoza katika taifa. Jamani ukosefu wa lishe bora katika mkoa ambao unalisha nchi nzima hilo halikubaliki," anasema Dk. Mpango.

Hapo anawataka viongozi mbalimbali wa dini, serikali na taasisi mbalimbali walivalie njuga suala hilo kwa kuhimiza elimu ya lishe.

"Chakula kipo,matunda yapo,maziwa yapo,dagaa zipo,nyama,asali, mahindi, maharagwe, mchele,samaki kila kitu kipo hapa hii ni paradiso kabisa," anasema Dk. Mpango.

Hapo anawataka pia walimu shuleni, kuhimiza matumizi ya vyakula bora na 'sio ili mradi kula kwa kujaza tumbo.'



# LATRA kukagua mradi reli kisasa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA), imejipanga kufanya ukaguzi maalum kwa ajili ya kuuthibitisha mradi wa reli ya kisasa (SGR) katika mwaka wa fedha 2022/23.

Vilevile, inatarajia kutunga kanuni za kudhibiti usalama wa abiria, mizigo na kupanga nauli za treni hiyo.

Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo, akizungumza juzi na waandishi wa habari, alisema mamlaka hiyo imepewa jukumu hilo la kutoa ithibati ya miundombinu na vitendea kazi vya mradi huo.

"Hivyo baada ya TRC kupata vichwa na mabehewa, kazi hiyo itaanza mara moja ili kubaini changamoto kabla ya treni kuanza ili kuzuia ajali," alisema.

"Tumejipanga kupitia hasa kwenye madaraja ambayo yamekuwa changamoto. Reli yenyewe, mifereji ya maji na viunganisho ni eneo ambalo tutaliangalia kwa makini kwa kuweka kanuni," aliongeza.

Kuhusu nauli, alisema yatawasilishwa mapendekezo ya nauli na yatapangwa kulingana na mapendekezo na maoni ya wadau.

Pia alisema mamlaka itafanya ukaguzi mbalimbali kwenye miundombinu ya reli za Shirika la Reli Tanzania (TRC) na Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia (TAZARA) ili kubaini mapungufu yanayoweka kuharakisha usalama wa treni.

Pia alisema LATRA imejipanga kuandaa kanuni za kutunza mazingira na uendeshaji wa reli kutokana na kuwapo kwa wimbi la wafanyabiashara kuvamia ushoroba wa reli.

"Pia tutatoa mafunzo kazini kwa wafanyakazi muhimu kwa usalama ili kuzuia ajali.

Mkurugenzi huyo alisema iliundwa timu ya wataalamu kwa ajili ya majadiliano na kampuni ya UBER Tanzania kulingana na hoja zao.

Alisema kuna hoja mbalimbali ikiwamo mapunjo ya fedha kwa madereva hivyo majadiliano yatakapofikia ukingoni mamlaka hiyo itatoa maamuzi.

Awali, alisema wamepokea mapendekezo ya Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) kuhusu kuanzisha usafiri wa waya ili kuongeza vivutio vya utalii.

Naye Mkurugenzi wa Udhibiti wa Usafiri wa Reli wa mamlaka hiyo, Hanya Mbawala, alitoa rai kwa wananchi kwamba treni ya mwendo kasi itakavyoanza majaribio asikatishe mtu wala mfugo kwa kuwa ni hatari.

"Asitokee mtu akakatisha maana hii treni itakuwa kwenye majaribio unaweza kuiona ipo mbali kumbe imefika, tunaomba sana wananchi wazingatie hili,"alisema.



Mkuu wa Idara ya Mazingira na Taka Ngumu, Dickson Kimaro, akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika jijini Dodoma jana, wengine waliokaa kutoka kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, Meya wa Jiji, Prof. Davis Mwamfupe na Naibu Meya, Emmanuel Chibago. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Nchemba ataka ma- RC kusimamia Sensa ya Watu na Makazi kwa weledi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba, amewaagiza wakuu wa mikoa na kamati za sensa wilaya kusimamia ipasavyo Sensa ya Watu na Makazi iaayofanyika Agosti 23, mwaka huu, ili kupata takwimu sahihi zitakazoiwezesha serikali kujibu kero mbalimbali za wananchi.

Amesema moja ya sababu zinazokabili nchi changa duniani ni ukosefu wa takwimu sahihi ambazo zingetumika kujibu kero zinazowakabili wananchi.

Dk. Nchemba alitoa maagizo hayo juzi jijini hapo alipokuwa akifunga mafunzo ya wakufunzi wa sensa ya watu na makazi ngazi ya mkoa kitaifa.

Alisema wakuu wa mikoa na kamati za sensa za wilaya zinapaswa kusimamia sensa ya watu na makazi ili ifanyike kwa ufanisi na kuipatia serikali takwimu sahihi.

"Niwaagize wakuu wa mikoa pamoja na kamati za sensa wilaya kuhakikisha mnakwenda kusimamia jambo hili kwa ukaribu sana na atakayeshindwa atakuwa kajipunja mgawo wa bajeti yake," alisema Nchemba.

Pia alisema serikali imewekeza fedha nyingi ili kufanikisha sensa hiyo, hivyo ni wajibu wa kila mtu kuhakikisha jambo hilo linafanikiwa kwa asilimia 100.

"Sensa si ya serikali au Rais pekee yake. Hili ni jambo la kila mmoja wetu kwani linahusu maisha ya watu, hivyo lazima tupate takwimu sahihi ili kila mmoja wetu apate kile alichostahili si kutumia bajeti ya mtu mwingine," alisisitiza.

Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi Tanzania Bara, Anne Makinda, aliwataka wakufunzi hao waliohitimu kwenda kuwafundisha makarani kutekeleza jukumu hilo kwa uzalendo mkubwa.

"Nawaombeni mwende kuwafundisha makarani kile ambacho mmekipata kutoka kwa wakufunzi wenu na muwe wakali kwa mtu yeyote ambaye ataonekana kuingia katika kundi hili la makarani 'kinamna namna'. mwondoeni mara moja kwani sensa ni kila kitu kwetu ni maisha yetu," alisema Makinda.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema sensa ni takwa la kisheria ambalo linamtaka kila Mtanzania kutoa takwimu zake ili kuiwezesha serikali kutekeleza wajibu wake wa kuondoa kero katika jamii.

"Sensa ni takwa la kisheria si hiari. Kila mtu anatakiwa kutoa taarifa zake kwa serikali ili serikali ichukue jukumu la kutekeleza mipango ya maendeleo kwa wananchi wake.

Lakini sensa ni takwa na Umoja wa Mataifa ambalo linataka sensa ikidhi matakwa ya kimataifa na mkishindwa kufanya hivyo sensa yenu inakataliwa.

"Nchi kama Nigeria ilifanya sensa yake lakini ilikataliwa na Umoja wa Mataifa kuwa haijakidhi vigezo, hivyo sisi tunataka kupata kitu ambacho hakina maswali na nikuhakikishe mgeni rasmi sisi Tanzania tuko vizuri," alisema Dk. Chuwa.

Dk. Marwa Majaliwa, kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa linajihusisha Idadi ya Watu (UNFPA), alisema hadi sasa wameshaisaidia Tanzania Sh. bilioni sita ambazo zinatumika katika maandalizi ya sensa.

# Waziri aagiza mfumo gesi soko la machinga

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, ameagiza kufungwa kwa mfumo wa kusambaza gesi asilia katika soko la kisasa jipya la Machinga linalojengwa jijini Dodoma ili kutunza mazingira.

Akizungumza jana alipotembelea soko hilo ili kuangalia suala la uhifadhi mazingira lilivyozingatiwa kabla ya kukamilika kwake, Dk. Jafo alimtaka Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma kuwasiliana na Mtendaji Mkuu wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) ili katika mfumo huo waweke mtungi mkubwa wa gesi soko hilo.

"Kama mtu anapika pale chakula lazima uwapo utaratibu wa gesi maana mpango wa serikali ni kuwa na matumizi ya nishati mbadala ya mtungi mkubwa ambao watu watafungiwa mita na watalipia kiwango watakachotumia. Kwa hiyo mkurugenzi wasiliana na mkurugenzi wa TPDC ili mfungiwe mfanane na soko la Feri," alisema na kuongeza kuwa gesi ni mkombozi wa uhifadhi mazingira.

"Ofisa Mazingira wa Jiji hakikisha kunakuwapo na msimamizi wa mazingira ya soko hili ili ziwapo bustani na miti ya kupendeza ili soko liwe na ajenda ya hadhi iliyopo," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alisema Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, anatarajiwa kuweka jiwe la msingi kwenye soko hilo, mwezi Agosti, mwaka huu. Alisema wanatarajia hivi karibuni kuanza kupanga wafanyabiashara kwenye soko hilo.

Naye Mkuu wa Idara ya Mazingira wa Jiji, Dickson Kimaro, alisema watahakikisha wanatekeleza maagizo ya waziri na kuweka utaratibu mzuri wa utiririshaji maji.





## Wachimbaji wapaza sauti kukosa maeneo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WACHIMBAJI wadogo wa dhahabu katika Wilaya ya Chunya, wamesema wanakosa maeneo ya kufanyia kazi kutokana na maeneo mengi kumilikiwa na wachimbaji wakubwa.

Kutokana na hali hiyo, wameiomba serikali kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya kundi hilo kufanyia shughuli zao ili kuondoa migogoro na wachimbaji wakubwa.

Wachimbaji hao waliyasema hayo juzi wakati wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Wachimbaji Wadogo uliokuwa na lengo la kuchagua viongozi wa mafundi wa kujenga migodi.

Katibu wa chama hicho mkoani Mbeya, Bonface Natai, alisema maeneo mengi yenye miamba yenye dhahabu, yanamilikiwa na wachimbaji wakubwa wenye leseni, hivyo kusababisha wachimbaji wadogo kukosa maeneo.

Alisema imekuwa ikiibuka migogoro ya mara kwa mara baina ya wachimbaji wadogo na wakubwa kutokana na kuingiliana kwenye maeneo hayo.

"Kila sehemu ukienda unakuta kuna mchimbaji mkubwa ana leseni ya kuchimba. Hali hii inasababisha wachimbaji wadogo kukosa maeneo ya kuwatosheleza kwa ajili ya shughuli zao," alisema Natai.

Baadhi ya wachimbaji wadogo wilayani Chunya, walisema wamekuwa wakishindwa kuendesha maisha yao kwa sasa kutokana na kukosa maeneo ya kuchimba dhahabu.

Mmoja wa wachimbaji hao, Juma Said, alisema wamiliki wengi wa leseni wanapenda kuwaajiri vijana wa wilaya hiyo na hawako tayari kuona maeneo yao yanachimbwa na wachimbaji wadogo hata kama hawajay-

# Watembea masafa kufuata huduma za afya

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

WAKAZI wa Kijiji cha Ngeleka, Kata ya Kisegese, Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe, wanalazimika kutembea umbali wa zaidi ya kilomita tano kwenda kutibiwa kwenye vituo vya afya vya kata jirani ya Ntaba au wilayani Kyela kutokana na kukosa huduma hiyo jirani.

Kutokana na hali hiyo wananchi hao wameamua kuchangishana fedha na kuanza ujenzi wa zahanati kijijini hapo na hadi sasa imefikia hatua ya uezekaji huku vifaa vyote vya ujenzi wakiwa wanabeba kichwani kutokana na kutokuwapo kwa miundombinu ya barabara.

Waliyasema hayo juzi wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Ujenzi, Atupele Mwakibete, alipotembelea kijijini hapo kwa nia ya kukagua shughuli za maendeleo zinazofanywa na wananchi hao.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi hao, Diwani wa Kisegese, Brighton Kala, alisema kata hiyo tangu ianzishwe na serikali miaka 10 iliyopita, haijawahi kuwa na Zahanati wala Kituo cha Afya, hali ambayo inasababisha upatikanaji wa huduma za afya kuwa mgumu.

"Kata yetu haijawahi kuwa na Zahanati wala Kituo cha Afya tangu kuanzishwa kwake. Zahanati hii iliyoanza kujengwa na wananchi wa kijiji hiki cha Ngeleka ndiyo inakuwa ya kwanza kwenye kata yetu, hivyo tunaiomba serikali itusaidie kuikamilisha lakini pia uwepo mpango wa kuanza ujenzi wa Kituo cha Afya kwenye kata hii," alisema Kala.

Alisema wananchi hao wanakabiliwa na ukosefu wa miundombinu ya barabara, umeme na maji hali ambayo inasababisha maisha yao kuwa magumu.

Kala alisema hata ujenzi wa Zahanati hiyo, wananchi wamelazimika kubeba vifaa vyote kichwani na kuvipeleka eneo la ujenzi kutokana na kutokuwapo barabara inayofika mpaka kwenye Zahanati hiyo.

Alimwomba Naibu Waziri huyo kusaidia ujenzi wa miundombinu ya barabara mpaka mahali ilipo Zahanati ili kurahisisha shughuli za ujenzi na pia wananchi watakaokuwa wanahitaji huduma wafike kirahisi.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Busokelo, Nuru Mwendapole, alisema baada ya wananchi kuanzisha mradi huo wa Zahanati, tayari serikali kupitia Halmashauri ya Busokelo imeshapeleka Sh. milioni 75 ili kusaidia ukamilishaji wa Zahanati hiyo.

"Halmashauri imeshatoa fedha kiasi cha Sh. milioni 75 kwa ajili ya kuunga mkono jitihada hizi za wananchi. Kwa kuwa wao wamejenga wenyewe mpaka hatua hii, fedha zilizotolewa zitatumika kupaua na kukamilisha ujenzi wote mpaka Zahanati hii itakapokuwa imeanza kutoa huduma," alisema Mwendapole. Alisema tayari halmashauri imeshaandaa wataalam wa afya watakaokwenda kwenye Zahanati hiyo kwa ajili ya kutoa huduma za afya kwa wananchi punde tu ujenzi utakapokamilika.

Kuhusu kero hiyo, Naibu Waziri Mwakibete ambaye pia ni Mbunge wa Busokelo alisema ataendelea kushirikiana na wananchi hao kuhakikisha Zahanati hiyo inakamilika na kuanza kazi ili kuwasogezea huduma za afya karibu.

Mwakibete alichangia mifuko 100 ya saruji papo hapo ili itumike kukamilisha ujenzi wa Zahanati hiyo, huku akiahidi kufuatilia kwenye taasisi husika upatikanaji wa miundombinu ya maji, umeme na barabara.

"Zahanati ni taasisi ya umma, uwepo wake katika eneo hili inatulazimisha sisi viongozi, na wala si hiari kuhakikisha tunapeleka maji, umeme na barabara bila kuchelewa," alisema.

Mwakibete alitumia fursa hiyo kuagiza Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) Wilaya ya Rungwe kuanza mchakato wa kulima barabara kuelekea kwenye Zahanati hiyo.




Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, akizungumza na wakazi wa Kata ya Kiwira katika Halmashauri ya Rungwe juzi aliposimama kuzungumza nao baada ya kukamilisha ziara ya kukagua miradi katika Halmashauri ya Kyela, Kusokelo na Rungwe. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wenye ualbino wafurahia kushirikishwa sensa

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

CHAMA cha Watu wenye Ualbino Tanzania (TAS) katika Mkoa wa Mbeya, kimesema sensa ya watu na makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti 23 mwaka huu, itasaidia kupata takwimu sahihi za kundi hilo kwa kuwa kwa sasa hawajui idadi yao.

Mwenyekiti wa chama hicho, Bruno Mwakyoma, aliyasema hayo juzi wakati wa kufunga mafunzo ya wakufunzi wa sensa ngazi ya wilaya katika mkoa wa Mbeya huku akibainisha kuwa kwa muda mrefu walikuwa wanashindwa kupata takwimu sahihi.

Alisema awali walikuwa wanatumia takwimu za makadirio ambazo kuna uwezekano si sahihi kutokana na wengine kuzaliwa, wengine kufa na wengine kuhamia au kuhama ndani ya mkoa na kwenda kuishi maeneo mengine.

Kitendo cha kutokuwa na takwimu sahihi, alisema kinawafanya washindwe kudai baadhi ya haki zao na kwamba baada ya sensa ya mwaka huu, watakiwa na nafasi ya kujua idadi yao, hivyo kuitumia katika kudai haki.

"Sisi kwenye mkoa wa Mbeya tumekuwa tukitumia takwimu za makadirio kwamba tuko zaidi ya 270 lakini takwimu hizi si halisi na hazitusaidii. Kupitia sensa ya mwaka huu, tunaamini tutapata takwimu sahihi na zitatusaidia kwenye harakati zetu," alisema Mwakyoma.

Alisema kwenye dodoso kuu la sensa kuna maswali 10 ambayo yanawahusu watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali wakiwamo wenye ualbino na wa viungo, hivyo akaipongeza serikali kwa maandalizi mazuri.

Katika hatua nyingine, Mwakyoma ambaye ni miongoni mwa wakufunzi wa sensa hiyo, aliishukuru serikali kwa kulitambua kundi hilo na kuliweka kuwa miongoni mwa makundi yatakayoshiriki kwenye sensa hiyo. Mratibu Msaidizi wa Sensa Mkoa wa Mbeya, Juma Maduhu, alisema katika mkoa wakufunzi ngazi ya wilaya waliothiriki mafunzo hayo wako 300 ma kwamba watapelekwa katika halmashauri zote za mkoa.

Alisema wakufunzi hao wamepatiwa mafunzo hayo kwa siku 21 zikiwamo siku tatu za kufanya majaribio ya kuhesabu watu kwenye vijiji na mitaa mbalimbali ndani ya Jiji la Mbeya na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Alisema wakufunzi hao watatoa mafunzo kwa zaidi ya makarani 7,000 watakaofanya kazi ya kuhesabu watu kwa siku 11 za sensa zikiwamo za mbili za kujaza dodoso la huduma za jamii na tatu za kujaza majengo.

"Hawa wakufunzi wamepikwa vizuri sana na wamefanya mitihani ambayo wote wamefaulu vizuri. Kwa sasa tunajiandaa kuwasambaza kwenye maeneo yote ya halmashauri zetu kwenda kuwafundisha makarani," alisema Maduhu.

Kuhusu kuwahesabu watu wenye ulemavu, Maduhu alisema makarani watakuwa wanahoji maswali kuhusu aina ya ulemavu ambao hauonekani lakini kwa ulemavu ambao unaonekana watajaza bila kuhoji.

Akifunga mafunzo hayo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Angelina Lutambi, aliwataka wakufunzi hao kwenda kufanya kazi kwa kuzingatia miiko ambayo wamefundishwa kwenye mafunzo hayo.

Dk. Lutambi alisema sensa ni muhimu kwa taifa kutokana na kusaidia kupata takwimu sahihi za wananchi ambazo zinasaidia kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.



## HABARI ZANZIBAR

# Mwinyi afichua siri ya kuwapo usalama, amani kisiwani Pemba

**Na Rahma Suleiman,** PEMBA

RAIS wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema kuwa kuimarika kwa hali ya usalama na amani kisiwani Pemba kunatokana na kuwapo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa iliyotokana na maridhiano ya kisiasa.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo juzi wakati akitoa majumuisho ya ziara yake katika Mkoa wa Kaskazini Pemba katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni, Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Alisema maridhiano hayo ya kisiasa yaliyofikiwa kati ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na ACT Wazalendo yamesaidia kuzika tofauti za kisiasa kisiwani Pemba.

Rais Mwinyi alisema amefurahishwa na hali ya ulinzi na usalama kisiwani hapa pamoja na ushirikiano mzuri kati ya wananchi na viongozi katika harakati za kimaendeleo bila kujali itikadi za kisiasa.

Dk Mwinyi alisema azma ya serikali yake ni kuhakikisha hadi kufikia mwaka 2025 uchumi wa Pemba unaimarika kama ulivyo wa Unguja.

Alisema hatua za serikali kuifanya Pemba kuwa eneo maalum la uwekezaji zimeanza kuleta matumaini mazuri na tayari wameshajitokeza wawekezaji wengi kutaka kuwekeza.

Miongoni mwa uwekezaji huo, alisema ni kujenga kiwanja cha ndege cha Pemba, mradi wa barabara ya Wete Chake pamoja na barabara ya Chake hadi Mkoani pamoja na barabara za ndani.

Alipongeza amani iliyoko kisiwani Pemba na kuwapongeza wananchi wa kisiwa hicho kwa hatua yao hiyo na kueleza kwamba kumeundwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ili wananchi waishi kwa amani, umoja na upendo.

Dk. Mwinyi alilitaka Baraza la Mji la Wete na Halmashauri ya Micheweni zijipange vizuri katika makusanyo na matumizi kwa sababu fedha nyingi zaidi zinahitajika katika miradi ya maendeleo kwa manufaa ya wananchi.

Alisema hatua hiyo inaweza kufanywa vizuri kutokana na kupungua kwa majukumu kutokana na kuondoa ugatuzi na kusisitiza kwamba Mabaraza ya Mji na Halmashauri ya Micheweni bado wanatakiwa kujikusanya vizuri kimapato.

Kwa upande wa sekta ya afya, ameridhika na ujenzi wa hospitali za wilaya za Wete na Micheweni na kusisitiza kwamba ni vyema sasa wakajipanga vizuri katika kuhakikisha vifaa tiba vinafika kwa wakati ili kufungwa na wananchi wakapata huduma.

Alisema haitakuwa busara kuwa na majengo mazuri lakini huduma zikawa mbovu huku akiwakumbusha kwamba majengo hayo mapya yanayojengwa yanahitaji huduma za maji, umeme na barabara zinazoelekea katika hospitali hizo na uzio huku akiwataka kupanga bajeti ya ziada.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza wakati alipotembelea ujenzi wa mradi wa tangi la kuhifadhia maji eneo la Kilindini Mkoa wa Kaskazini Pemba. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waziri ahimiza uzalishaji mazao ya viungo wakulima

**Na Rahma Suleiman,** PEMBA

WAZIRI wa Kilimo, Mifugo na Umwagiliaji, Shamata Shaame Khamis, amewataka wakulima wa mazao ya viungo kuongeza uzalishaji ili kuyafikia mahitaji ya soko la bidhaa hizo.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza katika ziara ya Rais Dk. Mwinyi alipowatembelea wajasiriamali wa wilaya ya Micheweni kisiwani Pemba ambao wamepatiwa mikopo kupitia fedha za ahueni za UVIKO-19 zilizotolewa na serikali.

Waziri alisema mikakati ya serikali ya Zanzibar ni kuongeza thamani kwa mazao ya viungo ambayo ndiyo kipaumbele cha kwanza ili kurudisha hadhi ya Zanzibar kuwa kituo kikuu cha uzalishaji na usafirishaji wa mazao hayo.

Alizipongeza asasi za kiraia pamoja na Umoja wa Ulaya (EU) kwa mikakati yake ya kuhamasisha wakulima kulima mazao ya viungo ambayo soko lake ni la uhakika.

"Nachukua nafasi hii kuzipongeza asasi za kiraia pamoja na Umoja wa Ulaya (EU) kwa kazi kubwa za kuhamasisha wakulima kuhakikisha wanalima mazao ya viungo ambayo soko lake lipo la uhakika," alisema.

Naye Waziri wa Kazi na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema katika mikakati ya kuwainua wajasiriamali katika kazi za ubunifu na uzalishaji, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imekubali kutoa Sh. Bilioni 3.6 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya uzalishaji na kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa nchini. Alisema wajasiriamali wanahitaji vituo vya uzalishaji utakaosaidia na kuongeza thamani ya uzalishaji wa mazao mbalimbali ya kilimo kwa ajili ya kuingia sokoni.

Alisema hiyo ni sehemu ya mikakati ambayo inakwenda kufungua milango ya kuwainua wajasiriamali kutokana na bidhaa wanazozalisha ikiwemo kuangalia ubora wake.

"Mheshimiwa Rais, nataka niwajulishe wananchi kwamba Benki ya Maendeleo ya Afrika wamekubali kutupa Sh. bilioni 3.6 kwa ajili ya kujenga vituo vya ubunifu na kuongeza thamani ya uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya kuingia sokoni," alisema.

Pia alisema ujenzi wa kiwanda cha usarifu na kuongeza thamani ya mwani kinatarajiwa kujengwa katika kisiwa cha Pemba eneo la Chamanangwe na kitawainua wakulima wa mwani kiuchumi.

Alisema kilio kikubwa cha wakulima wa mwani Unguja na Pemba ni kukosa soko la uhakika la bidhaa zao ambazo hazijasarifishwa na kuongezwa thamani ya ubora wake.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliwapongeza wanawake wa mkoa wa Kaskazini Pemba kwa kujitokeza kwa wingi kuchangamkia fursa za uwekezaji ikiwemo kuomba mikopo na kufanya biashara.

Aliwataka wananchi hao kuendelea kuchangamkia fursa ziliopo kwa wajasiriamali kwa kuchukuwa mikopo ambapo fedha zipo zimetengwa kwa walengwa.

# Hemed ataka utatuzi kero za mishahara

**Na Mwandishi Wetu**

WATENDAJI wakuu wa taasisi za serikali wametakiwa kumaliza changamoto zilizojitokeza kwa watumishi wa umma katika mabadiliko ya mishahara serikalini.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, aliyasema hayo katika kikao kazi kilichowakutanisha watendaji wakuu wa serikali kwa lengo la kujadili mabadiliko ya mishahara kwenye ofisi zao kilichofanyika katika ukumbi wa Sheikh, Idris Abdulwakil, Kikwajuni Zanzibar.

Alisema jambo hilo limeleta faraja kwa watumishi wa umma licha ya kuwapo kwa changamoto kadhaa zilizojitokeza na kueleza kuwa serikali haifurahishwi kuona zaidi ya asilimia 40 ya watumishi wana changamoto za ongezeko la mshahara na wengine kutofahamu kiasi walichoongezewa.

Hemed pia aliwataka makatibu wakuu kusimamia watumishi wenye malalamiko na kuyawasilisha Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kabla ya Agosti 10, mwaka huu ili kutatuliwa.

Kuhusu watumishi waliokosa nyongeza za mishahara, Hemed aliwataka viongozi hao kuwapatia stahiki na kuahidi kuwa serikali haitamwonea yeyote na kuwahakikishia kila mmoja atarejeshewa haki yake.

Pia aliwataka wakurugenzi wa utumishi kuwapatia elimu watumishi walio chini ya wizara zao ili wajue utaratibu uliotumika kuongeza mishahara na kuwataka kuwa wawazi juu ya madaraja ya watumishi na stahiki zao.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, alisema nyongeza hizo zimeanza mwezi huu kwa watumishi wote serikalini.

Alisema malalamiko yanaweza kutokea na kwamba wizara imeandaa dawati maalum la kupokea malalamiko na kuahidi kuwa watasimamia malalamiko hayo.

Naye Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mansura Mosi Kassim, alisema ongezeko la mshahara ni kwa watumishi wote na kuwaomba wakuu wa taasisi na maofisa utumishi wapitie na kuhakiki marekebisho hayo.

# Wajasiriamali kunufaika mikopo nafuu

**Na Mary Geofrey**

ASILIMIA 64 ya wajasariamali wanawake, wanatarajiwa kunufaika na mikopo ya riba nafuu baada ya kuzinduliwa kwa Mfuko wa Kuwezesha Wajasiriamali Wadogo Afrika (AFAWA).

Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Mfuko wa Dhamana Afrika (AGF) na Chama cha Benki Tanzania (TBA), ,juzi ilizindua mfuko huo jijini Dar es Salaam, wenye lengo la kuwakomboa wanawake wa Afrika kiuchumi.

Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, akizungumza muda mfupi baada ya kuzinduliwa kwa mfuko huo nchini, alisema ni fursa kwa wanawake kuinuliwa kiuchumi.

Alisema moja ya changamoto kubwa zilizokuwa zikiwakabili wanawake wajasiriamali ni mitaji licha ya serikali kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara.

"Sehemu kubwa ya wajasiarimali wenye matokeo chanya ni wanawake lakini ndio wahanga (waathirika) wakubwa ambao hawakopesheki na ndiyo sababu ya kuanzisha vikoba kwa ajili ya kuchangishana kupata mitaji," alisema.

"Jitihada hizi za wanawake za kuchangishana fedha za mitaji zimefanya serikali kuanzisha mpango huu mahususi kukopesha wanawake ili kukuza uchumi wao na wa taifa kwa ujumla," aliongeza.

Kigahe aliishukuru AfDB kwa kuja na mpango huo na Tanzania kuwa nchi ya kwanza kuuzindua. Alisema faida ya mpango huo ni benki kukimbilia kukopesha wanawake kwa riba nafuu na bila masharti magumu.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kundi la Mfuko wa Dhamana ya Afrika, Jules Ngankam, alisema: "Afrika ni bara changa zaidi duniani, lakini wakati huo huo, nusu ya watu haoni wanawake ambao wako mbali kufikia uwezo katika kushiriki uundaji wa thamani."

"Tunapoanza safari hii ya uwezeshaji wa kiuchumi kwa wafanyabiashara wadogo na wakati wanawake nchini Tanzania, kupitia mpango wa AFAWA wa dhamana ya ukuaji. tuna matumaini makubwa kuwa matokeohayo yatakuwa makubwa na ya muda mrefu na yatachochea ukuaji wa uchumi."

Meneja wa AFAWA, Esther Dassanou, alisema, asasi hiyo inafanya kazi moja kwa moja na taasisi zakifedha kote Afrika, ili kuimarisha uwezo wao wa kuhudumia soko la wanawake, kuruhusu wanawake kuongeza biashara zao.

Hadi sasa, Dola za Marekani milioni 520 zimeshapatikana kwa ajili ya kuweka dhamana kwenye benki ili wanawake wachukue mikopo na Dola za Marekani bilioni 64 zinahitajika kwa ajili ya wanawake wote wa nchi za Afrika.

Nchini Tanzania, fedha hizo zitawekwa kama dhamana kwenye benki za NMB, CRDB, Equaty na ABSA.



Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Kimataifa la Masula la Afya ya Uzazi na Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) Tanzania, Mark Bryan Schreiner akizungumza katika hafla ya kukabidhi vifaa tiba na jengo lililojengwa na shirika hilo kwa ufadhili wa nchi ya Finland, katika Hospitali ya Rufani ya Amana Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Marekani, Tanzania zajivunia ushirikiano kuinua vijana

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Marekani na Tanzania zimeadhimisha miaka mitano ya ushirikiano katika kuwawezesha vijana chini ya mpango wa 'Feed the Future Tanzania Inua Vijana'.

Kwa mujibu wa taraifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Ubalozi wa Marekani nchini jana, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof, Joyce Ndalichako, aliungana na Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), Kate Somvongisiri, kusherehekea mafanikio ya mpango huo.

Waziri pia aliongea na vijana hao ambao walitoa shuhuda za namna mpango huo ulivyowasaidia kuboresha maisha yao kiuchumi.

Aidha, mpango huo wa miaka mitano uliogharimu Dola za Marekani milioni 20, umesaidia vijana wa vijijini wenye umri wa kati ya miaka 15 hadi 35, unatekelezwa mikoa ya Iringa, Mbeya na Zanzibar.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa vijana hao ni wanaojihusisha na biashara ya kilimo na minyororo mingine ya thamani, katika kuongeza fursa zao za kiuchumi huku wakikuza uongozi na maisha bora.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, vijana wa Kitanzania wana nafasi kubwa katika maendeleo ya uchumi wa nchi yao, lakini kwa 800,000 wanaoingia katika nguvu kazi kila mwaka, ajira bado ni changamoto na kwamba mpango huo unashughulikia vikwazo kwa kuongeza fursa za kipato kwa vijana kupitia mafunzo ya kitaaluma na kuunganisha vijana na fursa za kazi rasmi na zisizo rasmi.

Mkurugenzi Mkazi wa USAID, Somvongsiri, alisema: "Tunajivunia kuwa mradi huu wa Inua Vijana umewafikia zaidi ya vijana 43,000 na kutoa zaidi ya Sh. bilioni 5.3 (Dola milioni 2.3) kama ruzuku kwa biashara za kilimo zinazomilikiwa na vijana."

# Mashahidi 54 kutoa ushahidi kesi uhujumu uchumi UDART

**Na Grace Gurisha**

VIELELEZO 153 na mashahidi 54 wanatarajia kutoa ushahidi dhidi ya aliyekuwa Mkurugenzi wa Mradi wa Usafirishaji wa Mabasi yaendayo Haraka (UDART), Robert Kisena (47) na wenzake katika kesi mbili za uhujumu uchumi zinazomkabili katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Hayo yalielezwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Pamela Mazengo na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ladslaus Komanya, akisaidiana wakili wa serikali, Thimotheo Mmari, wakati walipokuwa wakiwasomea washtakiwa maelezo ya mashahidi.

Komanya alidai kuwa hiyo ndiyo idadi ya mashahidi wanaotarajia kuwaita pamoja na vielelezo, kesi hizo mbili zilizofunguliwa katika Mahakama hiyo kwa hatua ya uchunguzi wa awali. Alidai, katika kesi hiyo ya kwanza namba 20, 2022 wanatarajia kuwaita mashahidii 24 na kuwasilisha vielelezo 58.

Inadaiwa vielelezo hivyo ni nyaraka mbalimbali zikiwamo taarifa za benki, mikataba waliyoingia washtakiwa na kampuni mbalimbali, maelezo ya maandishi ya mashahidi na ya washtakiwa, na hati za ukamatwaji wa washtakiwa na za upekuzi.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Charles Newe (48) Mkurugenzi wa UDART, mfanyabiashara John Samangu (66) na Mtunza Fedha wa UDART, Tumaini Kulwa (44).

Kwa pamoja, wanakabiliwa na jumla ya mashtaka 15, ambayo ni kuongoza genge la uhalifu na kughushi, kuwasilisha nyaraka za uwongo, utakatishaji fedha haramu na kuisababishia Udart hasara ya Sh. milioni 750 wakidaiwa kutenda makosa hayo kwa nyakati tofauti, Mei 25 na Julai 10, 2016.

Inadaiwa kuwa walihamisha pesa hizo kutoka katika akaunti ya UDART katika Benki ya NMB, tawi la Bank House, kwenda akaunti ya kampuni ya Long Way Engineering Ltd iliyoko Benki ya KCB.

"Wanadaiwa kuhamisha fedha hizi kwa madai ya kuzitumia kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya mabasi na uzio katika maeneo la Kimara, Kivukoni, Ubungo na Moroco, wakati wakijua sio kweli," alidai Komanya.

Katika kesi ya pili namba 21, 2022 iliyokuwa inasikilizwa na Hakimu Mfawidhi, Godfrey Isaya, serikali inatarajia kuwaita mashahidi 30 na kuwasilisha vielelezo vya nyaraka mbalimbali 95.

Katika kesi hiyo mbali na Kisena, Newe, Samangu na Kulwa, mshtakiwa mwingine ni Mkurugenzi wa kampuni ya Maxcom Africa, maarufu kama Maxmalipo, Juma Furaji (48).

Kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka 22 ya kuongoza genge la uhalifu, kughushi, kuwasilisha nyaraka za uwongo, utakatishaji fedha haramu na kuisababishia Udart hasara ya Sh. bilioni 4.5.

Inadaiwa walichukua fedha hizo kutoka akaunti ya UDART, Benki ya NMB, tawi la Bank House, na wanadaiwa kutenda makosa hayo kwa nyakati tofauti kati ya Juni 2015 na Aprili 30, 2016.

Kutokana na hatua hiyo, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu ilifunga majalada ya kesi hizo na pia ikiamuru kesi zihamishiwe Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, 'Mahakama ya Mafisadi' ambayo ndiyo ina mamlaka ya kusikiliza na kuamua kesi hizo.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya ...........TANGA**
**Kituo cha MJINI TANGA...........Mkoa...TANGA**
**Usimamizi wa Mirathi Na................153/2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: TWAHA MFAUME SALIMU**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA: RASHIDI BAKARI JAMBIA**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo 3/8/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
* Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
* Marehemu hakuacha wosia

**Imetolewa leo Tarehe 27/7/2022**

MAHAKAMA YA MWANZO MJINI TANGA
HAKIMU
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MJINI TANGA



**SHERIA YA UMILIKI WA ARDHI YA MWAKA 1999(SURA 113)**
**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA HAKI YA KUMILIKI ARDHI**
**MMILIKI ALIYEANDIKISHWA: JUMA HAMISI**
**ARDHI: KIWANJA Na. 280 KITALU "K"**
**ENEO LA MBAGALA**
**MANISPAA YA TEMEKE DAR ES SALAAM**

Taarifa inatolewa kwamba **BARUA YA TOLEO YA HAKI YA KUMILIKI ARDHI** iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa **NAKALA HALISI YA BARUA YA TOLEO YA HAKI YA KUMILIKI ARDHI.** Iwapo hakuna pingamizi litakalototolewa kwa muda wa siku 30 tangu tarehe ya taarifa hii ilipotangazwa katika gazeti.

**BARUA HALISI YA TOLEO** ikipatikana, irudishwe kwa **MKURUGENZI WA MANISPAA YA TEMEKE S.L.P.46343, DAR ES SALAAM.**

P.A. Masoy
AFISA ARDHI MTEULE
MANISPAA YA TEMEKE

# MAKAMBO: NIMEJIPANGA KUFANYA MAKUBWA BARA

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Yanga, Heritier Makambo, amesema amejipanga kufanya mambo mazuri na makubwa katika msimu mpya wa 2022/2023, ili kumshawishi kocha mkuu wa timu hiyo, Nesreddine Nabi kumpa nafasi kwenye kikosi cha kwanza.

Makambo ni mmoja wa wachezaji wa Yanga walioko kambini kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Makambo alisema msimu uliopita haukuwa mzuri kwake kwa sababu alishindwa kupata nafasi ya kucheza ila sasa anakuja kivingine kuhakikisha anaingia katika mipango ya Nabi.

Makambo alisema anaumia zaidi msimu uliopita haukuanza vizuri sana kwa sababu ya kukosa nafasi ya kucheza kama ilivyokuwa matarajio yake.

"Nimejipanga vizuri na kuhakikisha ninatumia Pre Season hii vizuri kwa kujituma na kufanya vyema katika programu zote tutakazopewa ili kumshawishi kocha (Nabi) aniamini na kunipa nafasi katika kikosi chake cha kwanza," alisema Makambo.

Alisema ushindani wa namba ni mkubwa sana kwa sasa hasa katika safu ya ushambuliaji kutokana na kuongezwa mastraika wapya kwenye dirisha la usajili linaloendelea.

"Nitapambana kuhakikisha ninakuwa sehemu ya kikosi cha kwanza cha timu, nimejipanga kukabiliana na ushindani wa kuania namba, ninajua nilipokwama msimu uliopita, lakini ninashukuru Mungu nilimaliza vyema kwa kupata nafasi ya kucheza mara nyingine," Makambo alisema.

Mkongomani huyo aliongeza maandalizi wanayoyafanya ni magumu kwa sababu wamejiandaa na ushindani unaotarajiwa kuonekana katika msimu mpya.

"Kila timu imejipanga kufanya vizuri, imefanya usajili mkubwa, hivyo tunajiandaa kukutana na changamoto katika kila mechi tutakayocheza, ligi itaendelea kuwa na ushindani kuanzia mechi ya kwanza," Makambo alisema.

Yanga itaanza msimu mpya kwa kukaribisha Simba katika mechi ya Ngao ya Jamii itakayochezwa Agosti 13, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.



Mwenyekiti wa Chama cha Netiboli Nchini (CHANETA), Dk. Devota Marwa (katikati), akielezea maandalizi ya Timu ya Taifa ya mchezo huo (Taifa Queens) itakayoshiriki mashindano ya dunia yatakayofanyika Afrika Kusini baadaye mwaka huu. Kushoto ni Kocha Mkuu wa Taifa Queens, Hafidh Ramadhani na Mjumbe wa CHANETA, Shukuru Kiwege. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Wanawake watakiwa kukuza vipaji*

**Na Sabato Kasika**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amewataka viongozi wanawake kuwa mstari wa mbele kuibua na kuendeleza vipaji vya watoto ili visipotee.

Gwajima alisema hayo jijini Dar es Salaam juzi katika warsha ya kuboresha haki za wanawake na vijana iliyoandaliwa na Chama cha Wanawake Wanasheria (TAWLA) na kufafanua baadhi ya watoto vipaji vyao vinapotea kutokana na madhila wanayopitia au kutotambuliwa na jamii inayowazunguka.

"Tumebaini vijana ambao wamekimbia nyumbani kwa wazazi wao, wapo wenye vipaji mbalimbali vikiwamo vya muziki, lakini wanakosa wa kuwashika mkono ili waweze kufikia ndoto zao," alisema Gwajima.

Waziri huyo aliwataka viongozi wanawake kuwa daraja la kubaini vipaji ili kusaidia nchi katika kuendeleza wasanii hao chipukizi kupata ajira. "Kuna watu Mungu amewaumba kazi yao ni sanaa ya kuburudisha, hivyo pamoja na kuwarejesha shuleni wapate elimu, tuibue vipaji vyao viimarike ili mwishowe waweze kutengeneza ajira kwa watu wengine," alisema waziri huyo.

Aliongeza kampeni hiyo inaweza kusaidia kukabiliana na ukatili wa kijinsia na kuukomesha, pia inasaidia kuibua vipaji vya watoto ambao baadhi yao wamekuwa wakikimbia vijijini na kukimbilia mijini lakini huishia mitaani.

## Usajili Zanzibar wapamba moto

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MCHAKATO wa kusajili wachezaji kwa ajili ya wanaotarajiwa kushiriki Ligi Kuu Zanzibar msimu 2022/2023 umekuwa mkubwa na huenda ukamalizika katika muda uliopangwa, imefahamika.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Zanzibar, Hashim Hashim, alisema zoezi hilo limekuwa na mwamko mzuri katika wiki hii na hali hiyo inafurahisha kwa klabu kuonyesha zinafanya vyema majukumu yake.

Hashim alisema mwamko huo unaendelea kujitokeza zaidi katika Kisiwa cha Pemba kwa viongozi wa vilabu kufanya usajili na uhamisho wa wachezaji kwa wakati.

"Kwa upande wa Unguja timu zinazoshiriki Ligi Kuu Zanzibar ndio zinajitokeza zaidi katika kufanya usajili ikilinganishwa na vilabu vitakavyocheza Ligi ngazi ya Kanda," alisema Hashim.

Aliongeza hata wachezaji wanaosajiliwa kutoka nje ya Zanzibar, usajili na uhamisho wake pia umefanyika mapema tofauti na inavyokuwa misimu iliyopita.

Dirisha la usajili na uhamisho wa wachezaji Zanzibar lilifunguliwa rasmi tangu Julai 15, mwaka huu na litafungwa ifikapo Agosti 20, mwaka huu.

## KMC FC yakataa makapi

**Na Adam Fungamwango**

MABOSI wa KMC FC wamesema wameanza kufanya usajili wa wachezaji wapya kwa kukamilisha taratibu na si kuchukua nyota walioachwa au ambao ni huru.

Ofisa Habari wa KMC FC, Christina Mwagala, alisema tayari kikosi chao kimeshaingia kambini kuanza maandalizi ya msimu mpya wakiwa na wachezaji wapya na wa zamani waliobakia kwa kufuata ushauri uliotolewa na benchi la ufundi.

"Kitu ambacho nataka niwatoe hofu mashabiki wa KMC ni unapotaka kujenga timu ni lazima ufanye maamuzi magumu, tumeacha wachezaji wengi kwa sababu tunataka kujenga timu imara, tumesajili wapya, tumesajili wenye ubora na hadhi ya kuichezea KMC, hatujasajili wachezaji changanyikeni, tumevunja mikataba kwenye klabu zao, " alitamba kiongozi huyo.

Aliongeza wakati wowote kuanzia sasa wataweka hadharani majina ya wachezaji wao wapya waliowasajili baada ya kukamilisha taratibu zinazotakiwa.

KMC imetangaza kuanza wachezaji 10 ambao ni Hassan Kapalata, Jean Baptiste Mugiraneza, Martin Kigi, Nickson Kibabage, Hassan Kabunda, Abbas Kapombe, Sudi Dondola, Denis Richard, Hassan kessy na Ally Ramadhani 'Kagawa'.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CHELSEA VS DE JONG

KIUNGO wa kati wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Frenkie de Jong angeondoka Barcelona na kujiunga na Chelsea, lakini klabu hiyo ya London haiko tayari kulipa kiasi kikubwa kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. (***Sport***)

### ATLETIKO YAMKATAA RONALDO

RAIS wa Atletico Madrid, Enrique Cerezo anasema hajui ni nani "aliyebuni" hadithi inayomhusisha mshambuliaji wa Manchester United, Cristiano Ronaldo na timu hiyo ya Hispania na kwamba "haiwezekani" mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno mwenye umri wa miaka 37 kujiunga nao. (***El Partidazo de COPE, via Eurosport***)

### WERNER ANUKIA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inavutiwa na mshambuliaji wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 26. (C***hristian Falk,Bild***)

### MARTIAL ATAJWA JUVENTUS

JUVENTUS inawataka Timo Werner na Anthony Martial mwenye umri wa miaka 26, kama hawataweza kukamilisha kumnasa mshambuliaji wa Hispania, Alvaro Morata (29) kutokea Atletico Madrid. (***Sky Sports***)

### SPURS MAMBO MAGUMU

MATUMAINI ya Tottenham Hotspur kumnunua kiungo wa kati wa Marekani, Weston McKennie mwenye umri wa miaka 23, yanaweza kuathiriwa baada ya mchezaji mwenzake wa Juventus, Paul Pogba wa Ufaransa (29) kupata jeraha la goti. (***Mail***)

### DUMFRIES ANUKIA CHELSEA

KLABU ya Chelsea imeelekeza mawazo yake katika kujaribu kumsajili beki Mholanzi, Denzel Dumfries mwenye umri wa miaka 26 kutoka Inter Milan. (***Evening Standard***)

### XAVI AMTAJA MESSI

KOCHA wa Barcelona, Xavi amesema "haiwezekani" kumsajili mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi kwa sasa kwani mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35 yuko chini ya mkataba na Paris St-Germain lakini akaongeza kuwa "tutaona katika siku zijazo". (***Goal***)

### SCHMEICHEL NJIA MOJA

GOLIKIPA wa Leicester City, Kasper Schmeichel amekubali kujiunga na klabu ya Nice ya Ufaransa, lakini uhamisho huo haujaidhinishwa. (***L'Equipe***)

### TIELEMANS BADO YUPO

MWENYEKITI wa Leicester City, Aiyawatt Srivaddhanaprabha amesema klabu hiyo haikuwa na ofa yoyote kwa kiungo wa kati wa Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 25, ambaye mkataba wake unamalizika msimu ujao wa joto. (***Metro***)


### AJORQUE AGEUKA LULU

KLABU ya Crystal Palace, Leicester City na Newcastle United zinafikiria kumnunua mshambuliaji wa Strasbourg, Ludovic Ajorque mwenye umri wa miaka 28. (***Football Insider***)

### VINAGRE KUTUA EVERTON

KLABU ya Everton inavutiwa na beki wa kushoto wa Sporting Lisbon, Ruben Vinagre mwenye umri wa miaka 23, ambaye aliwahi kuichezea Wolves. (***Liverpool Echo***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BARCELONA WAHAHA KUMRUDISHA MESSI

### ●●● Lakini Kocha Xavi aelezea kwa sasa mchakato huo hauwezekani, ila...

**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi anasemekana yuko katika hali mbaya na Barcelona huku kukiwa na uvumi wa kurejea Camp Nou siku zijazo.

Messi aliondoka kwenda PSG mwaka 2021 baada ya Barcelona kushindwa kumudu kuongeza mkataba wake, na kusaini mkataba wa miaka miwili katika klabu ya Parc des Princes ambao pia unajumuisha chaguo la kuongeza hadi mwaka 2024.

Tangu kuondoka kwake, kumekuwa na mazungumzo ya mara kwa mara ya kurejea Barcelona kwa raia huyo wa Argentina, huku Rais, Joan Laporta hivi majuzi akirejea uvumi huo kwa kukiri anataka kumrejesha Messi kwenye klabu hiyo.

Hii haikuwa mara ya kwanza kwa Laporta kuzungumza kuhusu Messi, na mchezaji huyo wa PSG hapo awali aliripotiwa kuchanganyikiwa na Barcelona kukataa kuacha kumzungumzia wakati wa mahojiano.

Wasiwasi uhusiano kati ya Messi na Barcelona unaweza usiwe na nguvu sana umeendelea tangu wakati huo na sasa Adria Albets ameelezea uhusiano wao kama 'umevunjika'.

Kocha wa Barcelona, Xavi amefanya kila awezalo kutuliza mazungumzo ya kutaka kumnunua Messi, akielezea dili la mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35 kuwa 'haliwezekani'.

"Tutaona katika siku zijazo, lakini sio wakati wa kuzungumza juu ya Leo, ni wakati wa kuzungumza juu ya wachezaji wa kusisimua tulio nao hapa," alisema Xavi kiungo wa zamani wa Barca akinukuliwa na 90min.

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,018,1

JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 28 JULAI 2022
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 28/07/22 | 19:00 | Paide Linnameeskond vs Ararat Armenia | 2.82 | 3.22 | 2.47 |
| 02. 28/07/22 | 19:30 | El Gouna vs Ismaily SC | 3.06 | 2.96 | 2.44 |
| 03. 28/07/22 | 19:30 | Farco FC vs Talaea El Gaish | 2.86 | 2.61 | 2.91 |
| 04. 28/07/22 | 19:45 | Maccabi Netanya vs Basaksehir | 3.02 | 3.22 | 2.33 |
| 05. 28/07/22 | 19:45 | Elfsborg vs Molde | 2.45 | 3.33 | 2.77 |
| 06. 28/07/22 | 20:00 | Dinamo Batumi vs Lech Poznan | 2.37 | 3.27 | 2.92 |
| 07. 28/07/22 | 20:00 | Olimpija Ljubljana vs Sepsi Osk | 2.52 | 3.19 | 2.78 |
| 08. 28/07/22 | 20:45 | Lechia Gdansk vs Rapid Vienna | 2.54 | 3.30 | 2.69 |
| 09. 28/07/22 | 21:00 | Hamrun Spartans vs Velez Mostar | 2.64 | 3.20 | 2.64 |
| 10. 28/07/22 | 21:00 | FC Vaduz vs Luka Koper | 2.58 | 3.24 | 2.68 |
| 11. 28/07/22 | 21:30 | Buducnost vs Breidablik | 2.39 | 3.44 | 2.78 |
| 12. 28/07/22 | 22:00 | Puskas Akademia vs Vitoria Guimaraes | 2.98 | 3.28 | 2.33 |
| 13. 28/07/22 | 22:00 | Coca Cola vs Zamalek | 3.05 | 3.05 | 2.38 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa, vodacom m-pesa, halopesa, airtel money, ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# AJAX WANAAMINI ANTONY HAONDOKI



**AMSTERDAM,** Uholanzi

KOCHA wa Ajax, Alfred Schreuder amesisitiza haamini, Antony anataka kuondoka katika klabu hiyo katika msimu huu wa joto, kwa mujibu wa 90min.

Inaeleweka mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil anabakia kuwa mmoja wa wanaohitajiwa sana na Kocha Erik ten Hag wa Manchester United, ingawa pendekezo lisilo rasmi la Mashetani Wekundu la pauni milioni 60 halitoshi kuwashawishi Ajax kumuuza.

Alipoulizwa kama anaogopa kumpoteza Antony msimu huu wa joto, Schreuder aliiambia Ziggo Sport kwamba, Ajax hawaamini watahitaji kumuuza winga huyo.

"Hapana, siogopi chochote," alisema. "Tunajua tuna wachezaji wazuri sana (hapa) na tunadhani tutaweka kikosi pamoja.

"Lakini najua, na kila mtu anajua, katika soka huwezi kujua."

Schreuder alisisitiza azimio hilo katika mahojiano mengine na De Telegraaf, na kuongeza Antony haonekani kama mchezaji anayevutiwa na uhamisho.

"Kwa ndani tumekubaliana tunataka kuweka kikosi cha sasa pamoja. Hakuna anayetaka kumuuza," bosi huyo mpya alisema.

"Antony anafanya kazi vizuri. Sina hisia yuko bize na uhamisho."

Licha ya msimamo wao hadharani, vyanzo vimethibitisha kwa 90min kwamba Ajax itakuwa tayari kumuuza Antony kwa bei inayofaa, huku miamba hao wa Uholanzi wakiaminika kushikilia mkataba wa karibu euro milioni 80.



# Kane asubiriwa Bayern Munich

**MUNICH,** Ujerumani

MKURUGENZI Mtendaji wa Bayern Munich, Oliver Kahn amekataa kuzungumzia uhamisho wa mshambuliaji wa Tottenham Hotspur, Harry Kane.

Kipa huyo wa zamani hivi karibuni alimwelezea Kane kama 'ndoto ya siku zijazo', wakati bosi wa Bayern Munich, Julian Nagelsmann pia ameweka hadharani jinsi anavyovutiwa na mshambuliaji huyo na kusababisha jibu la kutatanisha kutoka kwa bosi wa Spurs, Antonio Conte.

Akionekana na wasiwasi kuhusu kumkasirisha Conte kwa mara nyingine tena, Kahn alikataa kuvutiwa na mazungumzo kuhusu Kane alipoulizwa taarifa kuhusu nia ya Bayern Munich.

"Naweza kusema, Harry Kane ni mshambuliaji bora ambaye sasa yuko chini ya mkataba na Tottenham," alisema Kahn akiiambia Bild.

Conte ameeleza nia ya Bayern Munich kama 'uvumi pekee' na akasisitiza nia ya klabu hiyo kutaka kumweka Kane kwa siku zijazo.

Iliripotiwa na 90min mapema msimu huu wa joto kwamba, Spurs na Kane wana nia ya pande zote kujadili mkataba mpya, ingawa hakuna upande wowote ambao uko katika haraka ya kukaa na kurasimisha mambo kwa sasa.

16,895/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE


| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 30/07/22 | 17:00 | Cardiff vs Norwich City | 3.09 | 3.29 | 2.29 |
| 02. 30/07/22 | 17:00 | Millwall vs Stoke City | 2.26 | 3.34 | 3.09 |
| 03. 30/07/22 | 17:00 | Rotherham vs Swansea | 2.94 | 3.43 | 2.31 |
| 04. 30/07/22 | 17:00 | Wigan vs Preston | 2.40 | 3.19 | 2.99 |
| 05. 30/07/22 | 17:00 | Bristol Rovers vs Forest Green | 2.33 | 3.33 | 2.98 |
| 06. 30/07/22 | 17:00 | Carlisle vs Crawley Town | 2.27 | 3.28 | 3.13 |
| 07. 30/07/22 | 17:00 | Kilmarnock vs Dundee Utd | 2.26 | 3.24 | 3.19 |
| 08. 30/07/22 | 17:00 | St. Johnstone vs Hibernian | 2.98 | 3.08 | 2.47 |
| 09. 30/07/22 | 17:00 | Morecambe vs Shrewsbury | 2.94 | 3.29 | 2.38 |
| 10. 30/07/22 | 18:30 | GIF Sundsvall vs Varbergs Bois | 2.70 | 3.40 | 2.50 |
| 11. 30/07/22 | 19:00 | Odd Ballklubb vs Rosenborg | 3.03 | 3.38 | 2.28 |
| 12. 30/07/22 | 19:00 | Liverpool vs Manchester City | 2.62 | 3.18 | 2.45 |
| 13. 30/07/22 | 19:15 | Oostende vs Mechelen | 2.70 | 3.45 | 2.48 |
| 14. 30/07/22 | 19:30 | Enppi Club vs Al Masry Club | 3.02 | 2.98 | 2.48 |
| 15. 30/07/22 | 20:00 | Nimes vs Caen | 2.71 | 3.22 | 2.66 |
| 16. 30/07/22 | 20:00 | Le Havre vs Grenoble Foot | 2.33 | 3.08 | 3.33 |
| 17. 30/07/22 | 20:00 | US Quevilly Rouen vs Rodez Aveyron | 2.62 | 3.07 | 2.87 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 28/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 18:00 | 2850 | Astana vs Rakow Czestochowa | 3.13 | 3.28 | 2.25 |
| 19:00 | 3980 | Kisvarda FC vs Kairat Almaty | 1.87 | 3.39 | 4.15 |
| 19:00 | 4003 | Milsami Orhei vs KuPS Kuopio | 4.14 | 3.63 | 1.81 |
| 19:00 | 5257 | Gabala vs Videoton FC | 3.48 | 3.43 | 2.04 |
| 19:30 | 1749 | Farco FC vs Talaea El Gaish | 3.16 | 2.61 | 2.66 |
| 19:30 | 4378 | El Gouna vs Ismaily SC | 2.97 | 2.97 | 2.49 |
| 19:45 | 1578 | Maccabi Netanya vs Basaksehir | 3.24 | 3.19 | 2.24 |
| 19:45 | 3525 | Elfsborg vs Molde | 2.33 | 3.64 | 2.73 |
| 20:00 | 1327 | Apoel Nicosia vs Botev Plovdiv | 1.52 | 4.05 | 6.07 |
| 20:00 | 1880 | Djurgardens IF vs HNK Rijeka | 1.82 | 3.58 | 4.13 |
| 20:00 | 2751 | Lillestrom vs Seinajoen JK | 1.34 | 4.95 | 8.08 |
| 20:00 | 2793 | Slavia Prague vs ST Josephs FC | 1.03 | 13.09 | 50.34 |
| 20:00 | 3055 | Neftchi Baku vs Aris Limassol | 1.93 | 3.28 | 4.04 |
| 20:00 | 3336 | Olimpija Ljubljana vs Sepsi Osk | 2.73 | 3.24 | 2.53 |
| 20:00 | 3343 | Viborg FF vs Suduva | 1.31 | 5.05 | 9.09 |
| 20:00 | 3607 | CSKA Sofia vs Makedonija GjP | 1.42 | 4.44 | 7.06 |
| 20:00 | 3777 | Dinamo Batumi vs Lech Poznan | 2.33 | 3.28 | 2.98 |
| 20:00 | 3837 | Radnicki Nis vs Gzira United | 1.41 | 4.54 | 7.06 |
| 20:00 | 4014 | Viking vs Sparta Prague | 3.53 | 3.58 | 1.97 |
| 20:00 | 4845 | Levadia Tallinn vs Hibernians | 1.72 | 3.62 | 4.72 |
| 20:00 | 5582 | Newtown AFC vs Spartak Trnava | 4.95 | 3.89 | 1.64 |
| 20:00 | 5985 | FC Riga vs Ruzomberok | 1.96 | 3.29 | 3.90 |
| 20:30 | 2084 | Universitatea Craiova vs Vllaznia | 1.27 | 5.44 | 10.08 |
| 20:30 | 2180 | PAOK vs Levski Sofia | 1.47 | 4.14 | 6.66 |
| 20:30 | 3029 | Maccabi Tel Aviv vs Zira | 1.30 | 5.24 | 9.07 |
| 20:30 | 3674 | Steaua Bucuresti vs Saburtalo Tbilisi | 1.32 | 5.03 | 8.86 |
| 20:30 | 4184 | Panathinaikos vs FC Volendam | 1.54 | 3.84 | 5.31 |
| 20:45 | 3625 | Lechia Gdansk vs Rapid Vienna | 2.46 | 3.31 | 2.76 |
| 21:00 | 1111 | Brondby vs Pogon Szczecin | 2.25 | 3.23 | 3.17 |
| 21:00 | 1619 | FC Vaduz vs Luka Koper | 2.67 | 3.27 | 2.57 |
| 21:00 | 2716 | Konyaspor vs BATE Borisov | 1.38 | 4.73 | 7.45 |
| 21:00 | 2912 | Cukaricki St vs RFCU Luxembourg | 1.32 | 5.07 | 8.72 |
| 21:00 | 3265 | BSC Young Boys vs FK Liepaja | 1.08 | 9.33 | 30.43 |
| 21:00 | 3339 | NK Mura vs St Patricks | 1.90 | 3.38 | 4.04 |
| 21:00 | 4120 | KF Drita vs Royal Antwerp | 7.06 | 4.54 | 1.41 |
| 21:00 | 4323 | Laci vs Petrocub | 2.22 | 3.08 | 3.38 |
| 21:00 | 4483 | Sligo Rovers vs Motherwell | 3.63 | 3.38 | 2.01 |
| 21:00 | 4510 | Hamrun Spartans vs Velez Mostar | 2.73 | 3.24 | 2.53 |
| 21:00 | 5280 | Dinamo Minsk vs Hapoel Beer Sheva | 4.43 | 3.62 | 1.76 |
| 21:00 | 5955 | Shkendija vs Valmiera Fk/Bjss | 2.09 | 3.48 | 3.28 |
| 21:30 | 1495 | Buducnost vs Breidablik | 2.54 | 3.45 | 2.59 |
| 21:30 | 3906 | NK Osijek vs FK Kyzylzhar Petropavlovsk | 1.39 | 4.65 | 7.27 |
| 21:35 | 5424 | San Martin SJ vs San Martin Tucuman | 2.80 | 2.80 | 2.60 |
| 21:45 | 2204 | SP Tre Fiori vs B36 Torshavn | 4.12 | 3.52 | 1.84 |
| 21:45 | 4186 | FK Sloga Simin Han vs AZ Alkmaar | 6.48 | 4.66 | 1.43 |
| 22:00 | 2184 | Zrinjski Mostar vs KF Tirana | 1.67 | 3.74 | 4.95 |
| 22:00 | 2432 | Puskas Akademia vs Vitoria Guimaraes | 2.83 | 3.23 | 2.46 |
| 22:00 | 3384 | Coca Cola vs Zamalek | 3.05 | 3.05 | 2.38 |
| 22:00 | 4480 | Crusaders Belfast vs FC Basel | 8.08 | 4.95 | 1.34 |
| 22:00 | 5371 | Dunajska Streda vs Vikingur Gota | 1.40 | 4.64 | 7.06 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# LYANGA AONGEZA MZUKA STARS, MANULA MGONJWA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Soka ya Tanzania (Taifa Stars), Kim Poulsen amesema tayari kikosi chake kimeanza kuwa na kombinesheni katika safu ya ushambuliaji baada ya kumjumuisha straika, Danny Lyanga kwenye timu hiyo.

Taifa Stars inaendelea na mazoezi kwa ajili ya mchezo wa marudiano dhidi ya Somalia utakaochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), zitakazofanyika Algeria mapema mwakani.

Poulsen aliliambia gazeti hili ameendelea kukiimarisha kikosi chake kwa kumwongeza Lyanga ambaye msimu uliopita alikuwa na muunganiko mzuri akishirikiana na mshambuliaji mwenzake, George Mpole.

Kocha huyo alisema wachezaji wote wawili walikuwa na wakati mzuri katika msimu uliopita hivyo ana imani kucheza pamoja kutasaidia Stars kufanya vizuri katika mchezo wake marudiano dhidi ya Somalia.

"Lyanga ni mchezaji mzuri na kujumuisha ndani ya kikosi kutakuwa na faida kwa sababu ya mchezaji huyo na Mpole walicheza pamoja, pia walikuwa na pacha nzuri msimu uliopita, matumaini yangu hata huku watafanya vizuri," alisema Poulsen.

Aliongeza kuhusu hali ya David Luhende, alisema anaendelea vizuri na anatarajia kuwapo katika kikosi cha mchezo huo wa marudiano.

"Bahati mbaya majeruhi tuliyekuwa naye kwa sasa ni Aishi Manula, ana matatizo, aliumia katika mchezo uliopita na kupona kwake kutachukuwa muda mrefu kidogo," alisema kocha huyo.

Aliongeza anaendelea kuwaimarisha nyota wake ili wawe tayari kimwili kuelekea mchezo huo wa marajibio.



Mshambuliaji wa Timu ya Soka ya Tanzania (Taifa Stars), Dennis Kibu (kulia), akijiandaa kumtoka beki wa timu hiyo, Mohamed Hussein (Zimbwe Jr), katika mazoezi ya kuikaribisha Somalia hapo Jumamosi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: TFF**

# *Idadi maproo Bara kujadiliwa*

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), imesema suala ya wachezaji wa kigeni 12 waliosajiliwa kucheza wote katika mchezo mmoja litapelekwa kwenye kamati husika na huko ndiko hatima yake itaamuliwa, imeelezwa.

Ofisa Mtendeji Mkuu wa TPLB, Almasi Kasongo amekiri kupokea maoni mbalimbali ya wadau wa mpira wa miguu kwa ajili ya maboresho ya kanuni za Ligi Kuu msimu ujao wa 2022/2023, huku suala ya wachezaji 12 la kigeni likiwa miongoni mwa maoni hayo. "Ni mapema sana kusema, bado tupo kwenye huo mchakato, tutapeleka kwenye vikao halali vitaamua kwa sababu hili ni jambo la kanuni siyo jambo la Bodi, wala TFF (Shirikisho la Soka Tanzania), ni la wadau wenyewe, ambao ni klabu, ndiyo wataamua ni namna gani ambavyo wanataka wachezaji wa kigeni 12," alisema Kasongo.

Mbali na hayo, ofisa huyo alisema sekretarieti ya bodi hiyo itakutana kesho kupitia na kujidhihirisha maoni yote yaliyotumwa kama yapo sawa na kuyapekeka katika vikao husika.

"Si hilo la wachezaji wa kigeni tu, kumekuwa na maoni mengi na mitazamo tofauti kwa wadau wa soka ambayo wameyatuma kwetu, kila msimu unapoisha tunapokea maoni kwa ajili ya marekebisho," Kasongo alisema.

Baadhi ya timu zikiwamo Simba na Yanga zimekuwa zikilalamika zinaruhusiwa kuchezesha wachezaji wageni nane kati ya 12 wanaoruhusiwa kusajiliwa, kitu ambacho kinawanyima makocha wao fursa ya kupanga vikosi kwa kuangalia uwezo wa wachezaji.

Michezo

Alhamisi Julai 28, 2022

Nipashe





## Barcelona wahaha kumrudisha Messi



Rais wa Yanga, Injia Hersi Said (kushoto) na Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa SportPesa, Abbas Tarimba wakionyesha nakala baada ya kusaini mkataba mpya wa miaka mitatu na kampuni hiyo wenye thamani ya Sh. bilioni 12.33 jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SPORTPESA YAMWAGA MABILIONI YANGA

●●●Yaingia mkataba mpya wa Sh. bilioni 12.33 na kuahidi msimu ujao...

**Na Shufaa Lyimo**

KAMPUNI ya Michezo ya Kubahatisha ya SportPesa imeingia mkataba wa udhamini wa miaka mitatu na mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wenye thamani ya Sh. bilioni 12.33.

Mbali na kusaini mkataba huo wa udhamini, SportPesa pia jana ilikabidhi kiasi cha Sh. milioni 100 kwa mabingwa hao kutokana na kuchukua makombe matatu katika msimu uliopita ambao waliweka rekodi ya kutofungwa.

Akizungumza baada ya kusaini mkataba huo Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa SportPesa, Abbas Tarimba, alisema wameamua kusaini mkataba mpya baada ya ule wa awali wa miaka mitano ambao ulikuwa haujamalizika kwa sababu ya kuridhishwa na mafanikio waliyoyapata msimu uliopita.

Tarimba alisema ndani ya mkataba huo yameboreshwa mambo mengi ya msingi ambapo sasa kwa mwaka Yanga watapata Sh. bilioni 4 ambapo mkataba uliopita walipata Sh. bilioni 1.

Bosi huyo alisema mkataba huo unakwenda kuipa thamani Yanga ambayo msimu uliopita ndani ya miaka mitano bingwa alikuwa anapata Sh. milioni 100 na sasa bingwa ataondoka na Sh. milioni 150.

"Kampuni hii ikiwa kama mdhamini mkuu wa Yanga kama itafanikiwa kupata ubingwa msimu ujao itapata Sh. milioni 150, ikiingia hatua ya fainali kwenye Kombe la FA itapata Sh. milioni 75 lakini vilevile ikitwaa kombe hilo itapewa Sh. milioni 112, mtaona jinsi tulivyouboresha mkataba huu," alisema Tarimba.

Aliongeza juhudi za kupata mataji matatu bila kufungwa ndani ya msimu mmoja ni kitu ambacho hakikuwa rahisi.

Alisema timu hiyo imejipanga vizuri kuhakikisha msimu ujao utakaoanza Agosti 17, mwaka huu inaendeleza ushindani na kuongeza anawapongeza viongozi waliokuwa madarakani na wa sasa kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Alisema kampuni hiyo ilianza kwa malengo ya kusaidia maendeleo ya mpira nchini na kwa sababu hiyo ilisaini mikataba ya udhamini na klabu za Simba, Singida United na Yanga wakati timu hizo hazikuwa na hali nzuri kiuchumi.

Rais wa Yanga, Hersi Said alisema ameishukuru SportPesa kwa kuamua kusaini mkataba huo ambao amekiri haikuwa kazi rahisi kufikia makubaliano.

"Huu ni mwendelezo mzuri ambao tulianza nao miaka mitano iliyopita na leo (jana), tunasaini kuendelea nao kwa kipindi cha miaka mitatu," alisema Hersi.

Hersi alisema kampuni hiyo imekuwa sehemu ya mafanikio yao ambapo msimu uliopita walifanikiwa kutwaa mataji matatu kupitia udhamini huo na anaamini watafika mbali.

"Tumejipanga kutekeleza mambo yote yaliyoko ndani ya mkataba huu huku tukiahidi kuzindua jezi mpya za msimu ujao kesho (leo)," Hersi aliongeza.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Yanga, Senzo Mbatha, aliishukuru kampuni hiyo kwa kukubali kuwa mdhamini mkuu wa klabu hiyo na uhusiano huo uliodumu kwa miaka mitano.

"Mkataba huu utatekeleza mipango mipya ikiwamo mahusiano yatakayoleta manufaa ya pande zote mbili," alisema Senzo.

Aliongeza wamejipanga kufanya vizuri katika msimu ujao na kuiendesha klabu hiyo kisasa.

SportPesa pia walikuwa wadhamini wakuu wa Simba ambao hivi karibuni waliitangaza M-BET kuwa wadhamini wao wapya na wanatarajia kusaini mkataba mpya mapema mwezi ujao.

# Mastraika wamvuruga kocha Zoran

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Zoran Maki, ameonekana ni kama hajaridhishwa na mastraika walioko na badala yake ametaka kuongezewa washambuliaji wengine ili kikosi chake kiwe tishio katika msimu ujao.

Zoran ameweka wazi baada ya kubaini kuwa msimu uliopita Simba iliangushwa na safu hiyo.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema Zoran ameangalia kikosi cha msimu uliopita na kubaini kiliangushwa kwenye eneo hilo, hivyo ametaka aongezewe nguvu ili kuwa na kikosi kilichokamilika.

"Wanasimba wasiwe na wasiwasi, viongozi wao wapo kazini, wapo sokoni kusaka mastraika wengine wazuri, wakati huo huo mustakabali ya hawa tulionao ukiendelea kufanyiwa kazi ndani ya klabu, ukifahamika, kila mmoja atajulishwa," alisema Ahmed.

Taarifa zilizopatikana jijini zinasema, Meddie Kagere na Chris Mugalu huenda wakaachwa kutokana na si hawakufanya vyema msimu uliopita, lakini mpaka sasa wameshindwa kumshawishi Zoran katika mazoezi yanayoendelea huko Misri.

Hata hivyo, Ahmed alisema wachezaji hao bado wana mikataba na klabu hiyo na bado ni wachezaji wa Simba, hivyo hawezi kusema chochote kuhusu tetesi hizo mpaka pale uongozi na benchi la ufundi utakavyoamua vinginevyo.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alikaririwa akisema bado klabu hiyo haijafunga mchakato wa usajili na hata baadhi ya nyota walioko kikosini hawajafahamu hatima yao.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >